UTT AMIS
Asset Management and Investor Services

## KAMPUNI YA UWEKEZAJI YA UTT AMIS

# TAARIFA YA MWAKA YA MFUKO WA UWEKEZAJI WA WATOTO (WATOTO FUND)

Watoto Fund
Faraja kwa Watoto

## KWA MWAKA ULIOISHIA 30 JUNI 2025

# YALIYOMO

1. Ratiba na Ajenda za Mkutano....................ii
2. Muhtasari wa Mkutano Mkuu wa Kumi na Mbili....................1
3. Yatokanayo na Mkutano Mkuu wa Kumi na Mbili....................18
4. Barua ya Mwenyekiti wa Bodi....................21
5. Taarifa ya Mwangalizi wa Mfuko wa Watoto....................24
6. Taarifa ya Mkaguzi wa Hesabu za Mfuko....................26
7. Taarifa ya Hesabu za Mfuko....................29
8. Taarifa ya Meneja kuhusu Uwekezaji....................34
9. Jarida la Habari....................43

Watoto Fund
Faraja kwa Watoto

KAMPUNI YA UWEKEZAJI YA UTT AMIS
MKUTANO MKUU WA WAWEKEZAJI WA
MFUKO WA WATOTO JUMAPILI TAREHE
21 DISEMBA 2025 UKUMBI WA MIKUTANO
WA KIMATAIFA WA JULIUS NYERERE – DAR ES SALAAM

# RATIBA NA AJENDA ZA MKUTANO

| MTIRIRIKO WA SHUGHULI | | | |
|---|---|---|---|
| **S/N** | **MUDA** | **SHUGHULI** | **WAHUSIKA** |
| 1. | 06.30 - 08.00 | Kuwasili kwa Wajumbe na Kujiorodhesha | Wajumbe/Utawala |
| 2. | 08.00 - 08.10 | Matangazo na Shughuli za Utawala | MC/Utawala |
| 3. | 08.10 - 08.15 | Kuthibitisha Akidi na Kufungua Mkutano | Mwenyekiti wa Bodi |
| 4. | 08.15 - 08.30 | Utambulisho (Wakurugenzi, Uongozi na Watoa Huduma kwa Mfuko) | Mkurugenzi Mtendaji |
| 5. | 08.30 - 08.40 | Kupitia Muhtasari wa Mkutano Mkuu wa Kumi na Mbili | Wote |
| 6. | 08.40 - 08.55 | Kupitia Taarifa za Yatokanayo na Mkutano Mkuu wa Kumi na Mbili | Mkurugenzi Mtendaji |
| 7. | 08.55 - 09.25 | Barua ya Mwenyekiti kwa Wawekezaji | Mwenyekiti wa Bodi |
| 8. | 09.25 - 09.40 | Kupokelewa kwa Taarifa ya Mwaka<br>1. Mwangalizi wa Mfuko<br>2. Mkaguzi wa Hesabu<br>3. Taarifa ya Hesabu | <br>CRdB<br>KpMg<br>Mkurugenzi wa Fedha na Mipango |
| 9. | 09.40- 10.10 | Kupokea Taarifa ya Meneja kuhusu Uwekezaji | Mkurugenzi wa Uwekezaji |
| 10. | 10.10 - 10.30 | Kipindi cha Maswali na Majibu | Bodi/Watendaji |
| 11. | 10.30 -10.45 | Kufunga Mkutano | Mwenyekiti wa Bodi |

# 2 Muhtasari wa Mkutano wa Kumi na Mbili (12) wa Mwaka

# KUMBUKUMBU ZA MKUTANO WA KUMI NA MBILI (12) WA MWAKA WA MFUKO WA WATOTO ULIOFANYIKA TAREHE 17 NOVEMBA 2024 KATIKA UKUMBI WA MIKUTANO WA KIMATAIFA WA JULIUS NYERERE JIJINI DAR ES SALAAM

## WALIOHUDHURIA (Kiambatanisho "A")

### BODI YA WAKURUGENZI

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Prof. Faustin R. Kamuzora | - | Mwenyekiti wa Bodi |
| 2. | Dkt. Judika L. King'ori | - | Mjumbe wa Bodi |
| 3. | Bw. David E. Mwankenja | - | Mjumbe wa Bodi |
| 4. | Bw. Paul A. Maganga | - | Mjumbe wa Bodi |
| 5. | Bw. Simon M. Migangala | - | Mkurugenzi Mtendaji |

### WAJUMBE WA KAMATI ZA BODI YA WAKURUGENZI

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Dkt. Fortunatus. Magambo | - | Mjumbe wa Kamati ya Bodi |
| 2. | Bw. Lameck Kakulu | - | Mjumbe wa Kamati ya Bodi |

### WASIOHUDHURIA KWA TAARIFA

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Bi. Neema J. Jones | - | Mjumbe wa Bodi |
| 2. | Bw. Daniel Olesumayan | - | Mjumbe wa Kamati ya Bodi |

### WAALIKWA

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Bw. Amiri Juma Ally | - | Mwakilishi wa Msajili wa Hazina |
| 2: | Bi. Aisha Mbilikira | - | CMSA/ Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana |
| 3. | Bw. Frank Mboya | - | KPMG/Wakaguzi wa Hesabu za Mfuko |
| 4. | Bw. A. Meena | - | CRDB/ Waangalizi wa Mfuko |
| 5. | Bi. Sephania Shambwe | - | CRDB/ Waangalizi wa Mfuko |
| 6. | Bw. Mustafa Haji | - | CRDB/ Waangalizi wa Mfuko |

### MENEJIMENTI NA WAFANYAKAZI WA KAMPUNI YA UWEKEZAJI YA UTT AMIS

1. Bw. I. Wahichinenda
2. Bi. J. Msofe
3. Bi. S. Mgaya
4. Bw. D. Balima
5. Bw. D. Mbaga
6. Bw. S. Bujiku
7. Bw. S. Kaniki
8. Bw. R. Mwanga
10. Bw. P. Ndunguru
11. Bi. V. Abuogo
12. Bw. F. Bwalya
13. Bw. B. John
14. Bi. J. Mlimbila
15. Bw. M. Balati
16. Bw. H. Mnongane
17. Bw. B. Liwali
18. Bw. C. Chanjarika
19. Bw. J. Joseph
20. Bi. R. Maruma
21. Bw. J. Masoud
22. Bw. B. Lukinga
23. Bw. A. Mushi
24. Bw. W. Ramadhan
25. Bi. J. Njovu
26. Bi. V. Maheri
27. Bi. D. Milenge
28. Bi. W. Malya
29. Bi. H. Lashkoni
30. Bw. A. Mabruk
31. Bw. A. Ambari
32. Bw. J. Nyambo
33. Bw. S. Ivambi
34. Bi. S. Kapufi
35. Bi. Y. Masanyoni
36. Bi. A. Laurent
37. Bi. E. Simon
38. Bw. M. Mchanjila
39. Bw. J. Mwangomola
40. Bi. M. Minja
41. Bw. C. Josiah
42. Bi. M. Mashiku
43. Bw. F. Lushinge
44. Bi. D. David
45. Bw. S. Khatib
46. Bi. P. Kasilati
47. Bw. F. Mzoo
48. Bi. V. Mashindano
49. Bi. A. Omari
50. Bw. A. Kandila
51. Bw. A. Felecian
52. Bi. L. Malimiru
53. Bi. J. Mteri
54. Bi. A. Alex
55. Bw. D. Makassy
56. Bw. Straton Rugaitika
57. Bi. A. Kijaji
58. Bw. N. Mlembah
59. Bw. C. Kilawe
60. Bw. O. Mafuru
61. Bi. A. Kalinga
62. Bi. P. Kunambi
63. Bi. J. Kilimba
64. Bi. H. Swalehe
65. Bi. E. Kahabi
66. Bw. B. Raphael
67. Bw. S. Mahumi
68. Bw. L. Temela
69. Bw. N. Muhoji
70. Bi. A. Mwinuka
71. Bi. C. Ngunda
72. Bw. H. Njau
73. Bi. F. Mwalisito
74. Bi. T. Mpiluka

## 1.0 AKIDI NA KUFUNGUA MKUTANO

Mwenyekiti alifungua mkutano saa 08:45 Mchana kwa kuwakaribisha wajumbe walioweza kuhudhuria Mkutano wa 12 wa Mfuko wa Watoto. Hii ilikuwa baada ya wajumbe kupokea taarifa ya akidi, ambayo ilionesha kuwa Wajumbe wenye vipande waliohudhuria walikuwa 460 ambao majina yao yapo kwenye kumbukumbu hizi kama Kiambatisho "A". Mkurugenzi Mtendaji alitoa taarifa kwamba idadi ya Vipande vilivyoandikishwa vilikuwa 3,775,357.92 sawa na asilimia 12 ya jumla ya vipande vyote vya Mfuko kiasi cha Vipande 32,139,559.91. Taarifa iliendelea kueleza kuwa idadi hiyo ya vipande vilivyowakilishwa inakidhi akidi inayohitajika kulingana na Waraka wa Makubaliano (Deed of Trust) ya asilimia 10 ya jumla ya vipande vyote vya Mfuko na hivyo Mkutano ungeweza kuanza.

## 2.0 DONDOO/AJENDA ZA MKUTANO

Wajumbe walikubaliana na dondoo/ajenda zifuatazo:

1. Taarifa ya Akidi na Kufungua Mkutano
2. Kuthibitisha Dondoo/Ajenda za Mkutano
3. Utambulisho
4. Kuthibitisha Kumbukumbu za Mkutano Uliopita
5. Yatokanayo na Kumbukumbu za Mkutano Uliopita
6. Taarifa ya Mwenyekiti
7. Taarifa ya Mwangalizi wa Mfuko
8. Taarifa ya Mkaguzi wa Mfuko
9. Taarifa ya Hesabu za Mfuko
10. Taarifa ya Meneja wa Mfuko kuhusu Uwekezaji
11. Kipindi cha Maswali na Majibu
12. Kufunga Mkutano

## 3.0 UTAMBULISHO

Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Uwekezaji ya UTT AMIS aliwatambulisha Wajumbe wa Bodi ya Wakurugenzi ya Kampuni ya UTT AMIS, Wajumbe wa kamati za Bodi, na Wawakilishi wa Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA). Aliendelea kuwatambulisha pia Wawakilishi wa Benki ya CRDB ambayo ni Mwangalizi wa Mfuko, Wawakilishi wa Kampuni ya KPMG inayotoa Huduma za Ukaguzi wa Hesabu za Mfuko pamoja na Mwakilishi kutoka ofisi ya Hazina ambayo inasimamia Taasisi za Serikali ikiwemo UTT AMIS. Mkurugenzi Mtendaji alimaliza kwa kutambulisha Menejimenti ya UTT AMIS pamoja na wafanyakazi wote waliokuwepo Mkutanoni kwa ujumla.

## 4.0 KUTHIBITISHA KUMBUKUMBU ZA MKUTANO ULIOPITA

Baada ya kuzipitia kurasa zote za kumbukumbu za Mkutano wa kumi na moja, wajumbe kwa kauli moja walithibitisha na kuzipitisha kumbukumbu za Mkutano wa kumi na moja (11) uliofanyika tarehe 20 Novemba 2023.

## 5.0 YATOKANAYO NA KUMBUKUMBU ZA MKUTANO ULIOPITA

**Hapakuwa na yatokanayo na Mkutano wa Kumi na Moja (11).**

## 6.0. TAARIFA YA MWENYEKITI

6.1 TAARIFA YA MWENYEKITI

6.2 Mwenyekiti aliwasilisha taarifa ya Mfuko wa Watoto kwa mwaka wa fedha ulioishia Juni 30, 2024. Aliwakaribisha wajumbe kwenye Mkutano Mkuu wa 12 wa Mwaka wa Wawekezaji wa Mfuko wa Watoto.

6.1 Alianza kwa kumshukuru Mhe, Dkt, Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kumteua kuiongoza Bodi ya Wakurugenzi ya UTT AMIS. Pia aliwashukuru Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb), Waziri wa Fedha, Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha, Dkt Natu Mwamba na Msajili wa Hazina, Ndugu Nehemiah Mchechu kwa kumpatia miongozo mara tu baada kuteuliwa kuwa Mwenyekiti wa Bodi ya UTT AMIS. Aliwashukuru pia wawekezaji kwa kuendelea kuwa na Imani kubwa katika mfuko wa Watoto.

6.2 Mwenyekiti wa Bodi aliendelea kutoa shukurani kwa kumshukuru Mwenyekiti aliyemaliza muda wake, Ndugu Casmir Sumba Kyuki, kwa uongozi imara na kazi nzuri ya kuiongoza taasisi ya UTT AMIS na kuifanya kuwa moja kati ya taasisi zinazoongoza katika Soko la Mitaji na Dhamana nchini Tanzania na ukanda wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, na pia kumtakia afya njema na heri katika majukumu yake mengine.

6.3 Mwenyekiti aliwaeleza wawekezaji kuwa, kwa zaidi ya miaka 20 ya uwepo wa UTT AMIS, ni Dhahiri kuwa fedha nyingi zimewekezwa kwa niaba ya wawekezaji na kurudishwa kama faida. Aliendelea kuwaeleza kwamba, uwekezaji huu tulivu (Passive Investment) huwafanya wawekezaji kutengeneza faida huku wakiwa wamelala au wakiendelea kutekeleza majukumu mengine ya kimaisha. Mwenyekiti alimnukuu mwekezaji maarufu aliyefanikiwa sana, Ndugu Warren Buffet, ambaye aliwahi kusema, *"kama hutakuwa na namna ya kupata fedha wakati umelala, utafanya kazi mpaka utakapofariki."*

6.4 Aidha, Mwenyekiti aliwaeleza wawekezaji kuwa, kutokana na jitihada kubwa zilizofanywa na Menejimenti pamoja na wafanyakazi wote na usimamizi imara wa Serikali, hakushangazwa sana pale UTT AMIS ilipotangazwa kuwa mshindi wa jumla kwa taasisi zinazoendeshwa kwa ufanisi bora nchini Tanzania. Hakika alijisikia mwenye furaha pale alipokabidhiwa tuzo kutoka kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan jijini

Arusha, wakati wa mkutano wa Wenyeviti na Watendaji wakuu wa taasisi za umma tarehe 28 Agosti, 2024.

6.5 Taarifa ya Mwenyekiti iliendelea kueleza kuwa utendaji wa Mfuko wa Watoto uliendelea kuwa mzuri kwa mwaka wa fedha ulioishia 30 Juni 2024. Faida kwa wawekezaji ilikuwa kubwa ikilinganishwa na kigezo linganifu (Performance Benchmark) ikiwa ni wastani wa faida ya asilimia kumi na nne nukta moja (14.1%) ikilinganishwa na asilimia kumi na mbili nukta nne (12.4%) ya mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2023. Faida iliyopatikana iko sawa na maendeleo ya soko na ni kubwa kuliko kigezo linganifu cha asilimia 11.2% katika kipindi cha mwaka wa fedha kilichoishia tarehe 30 Juni 2024. Katika kipindi cha mwaka wa fedha ulioishia Juni 2024, thamani ya mfuko iliongezeka kutoka shilingi bilioni 10.7 iliyofikiwa Tarehe 30 Juni 2023 hadi Shilingi bilioni 18.9 tarehe 30 Juni 2024. Mwakilishi wa Mwenyekiti aliwaeleza wawekezaji kuwa, ongezeko hili la thamani ya Mfuko limetokana na faida nzuri inayopatikana, matumizi ya teknolojia katika kufanya miamala ya uwekezaji, kuongezeka kwa Imani na elimu juu ya faida zinazopatikana kupitia Mifuko ya uwekezaji wa pamoja.

6.6 Taarifa ya Mwenyekiti iliwajulisha wawekezaji kuwa pamoja na vihatarishi vitokanavyo na taharuki ya hali ya kisiasa na vita katika sehemu mbalimbali duniani, hali ya uchumi nchini Tanzania iliendelea kuimarika kwani ulikua kwa asilimia 5.1 kwa mwaka 2023 na unatarajiwa kukua kwa asilimia 5.4 kwa mwaka 2024. Ukuaji huu wa uchumi ni mzuri zaidi ya wastani wa ukuaji katika nchi za ukanda wa Jangwa la Sahara na nchi za ukanda wa Ushirikiano wa Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) ambao ni asilimia 3.4 kwa mwaka 2023 na makadirio ya asilimia 3.8 kwa mwaka 2024, kama ilivyokadiriwa na Shirika la Fedha Duniani (IMF). Pia, kwa mujibu wa taarifa za Benki Kuu ya Tanzania, mfumuko wa bei ulikuwa asilimia 3.1 mwezi Juni 2024 ikilinganishwa na matarajio ya kiwango kisichozidi asilimia 5.0 na matarajio ya nchi za ukanda wa Afrika Mashariki cha asilimia 8.0. Kwa kipindi cha mwaka mmoja uliopita viwango vya riba katika soko havikubadilika sana na hivyo kuashiria utulivu wa soko kwa ujumla. Kwa upande mwingine, thamani ya Shilingi ya Tanzania dhidi ya Dola ya Marekani ilipungua kwa kiwango cha asilimia 12.8 sababu kubwa ikiwa ni kubadilika kwa sera za nchi ya Marekani na madhara yatokanayo na taharuki ya vita katika bara la Asia.

6.7 Kuhusu maendeleo ya Soko la Mitaji na Dhamana ambalo utendaji wake hupimwa kwa kuangalia mabadiliko ya Fahirisi (Tanzania Share Index), imeonesha kuwa na maendeleo mazuri. Katika kipindi cha mwaka kilichoishia tarehe 30 Juni, 2024, kumekuwa na ongezeko la Fahirisi la asilimia 9.3 ambapo iliongezeka toka 4,091.8 tarehe 30 Juni 2023 hadi 4,475.2 tarehe 30 Juni 2024. Ongezeko hilo ni zaidi ya lile la tarehe 30 Juni, 2023 ambalo lilikuwa ni asilimia 4.1. Hii inamaanisha kuwa, kwa kipindi cha mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2024, bei za Hisa kwa ujumla ziliongezeka ikilinganiswa na mwaka uliopita. Sababu za kupanda kwa bei za Hisa kulichagizwa na utendaji mzuri wa Makampuni yaliyoorodheshwa katika Soko la Hisa la Dar es Salaam, kuongezeka imani kwa wawekezaji wa ndani na wa nje ya nchi na kuboreshwa kwa mazingira ya uwekezaji hapa nchini. Shukurani zilitolewa kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan na Serikali kwa ujumla kwa kuendelea kusimamia na kuweka mazingira bora ya biashara.

6.8 Wawekezaji walielezwa kupitia taarifa ya Mwenyekiti kuwa viashiria vya kiuchumi vinaonesha kwamba Kampuni ya uwekezaji ya UTT AMIS pamoja na Mifuko inayoisimamia imeendelea kufanya vizuri. Thamani ya Mifuko imeongezeka kutoka Shilingi trilion 1.5354 tarehe 30 Juni, 2023 hadi kufikia Shilingi trilion 2.2382 tarehe 30 Juni, 2024. Hili ni ongezeko la shilingi bilioni 702.8, sawa na asilimia 45.7 ikilinganishwa na ongezeko la shilingi bilioni 538.9, sawa na asilimia 54.0 kwa mwaka uliopita. Ongezeko la ukubwa wa Mifuko umetokana na ongezeko la faida iliyopatikana katika uwekezaji Pamoja na idadi ya Wawekezaji 79,519, sawa na asilimia 32 waliojiunga katika Mifuko kwa mwaka 2024 ikilinganishwa na Wawekezaji 47,480, sawa na asilimia 24 waliojiunga mwaka wa fedha uliopita. Kama nilivyosema hapo awali kwamba mifuko yote imetoa faida nzuri kwa wawekezaji wake. Faida kwa mfuko wa Watoto ilikuwa asilimia 14.1.

6.9 Mwenyekiti alieleza kuwa, Kampuni ya UTT AMIS imeendelea na awamu ya mwisho ya utekelezaji wa Mpango Mkakati wake wa miaka mitano unaoishia Mwezi wa Juni Mwaka 2024. Pia UTT AMIS ilitayarisha mpango mkakati mpya wa miaka mitano. Mpango mpya umejikita katika kuifanya UTT AMIS kuwa mshirika mkubwa zaidi katika soko la Mitaji na dhamana nchini Tanzania na ukanda wa Afrika Mashariki. Ili kuendana na kipindi cha mipango cha Serikali, Mpango Mkakati mpya utafanyiwa mapitio ndani 2024/2025 ili uweze kumalizika mwezi Juni 2030. Kati ya malengo yalioainishwa katika mpango mkakati mpya ni Pamoja na kukuza thamani ya mfuko kutoka shilingi Trilioni 2.238 cha sasa hadi shilingi Trilioni 7.5, na kuongeza idadi ya

matawi ili kusongeza huduma kwa wawekezaji nchini na nchi za Africa Mashariki Pamoja na nchi za ukanda wa nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara (SADC). Zaidi ya hapo, Mpango Mkakati unaonesha kuwa huduma kwa wawekezaji zitakuwa za kidijitali. UTT AMIS ndani ya mwaka huu wa fedha 2024/2025 imeanza na uboreshaji wa mifumo ili kuimarisha uwezo na kumudu kiwango kikubwa cha biashara. Mradi huu wa kuboresha mifumo unatarajiwa kukamilika ndani ya kipindi cha miezi kumi na mbili.

6.10 Aidha, Wawekezaji walijulishwa kuwa, kwa kipindi cha miaka mitano ya utekelezaji wa Mpango Mkakati wa Kampuni ya uwekezaji ya UTT AMIS unaoishia Juni 2024 kumekuwa na mafanikio makubwa zaidi ya ilivyotarajiwa. Thamani ya mifuko ilikisiwa kukua kutoka shilingi bilioni 290.7 tarehe 30 Juni 2019 mpaka shilingi bilioni 485.9 kabla ya kurekebishwa na kuwa shilingi bilioni 1,007.9 tarehe 30 Juni 2024. Hata hivyo, thamani halisi ya mifuko mpaka kufikia tarehe 30 Juni 2024 ilikuwa ni shilingi Trilion 2.2 ambayo ni mara mbili ya kiwango kilichotarajiwa. UTT AMIS itaendelea kuboresha huduma za uendeshaji kuwa za kisasa zaidi na kuhakikisha kuwa wawekezaji wanapata faida nzuri zaidi kadri ya maendeleo ya soko la Mtaji. Pia UTT AMIS inatarajia kuwafikia na kuwahudumia wawekezaji wengi zaidi nchini Tanzania, Ukanda wa Afrika mashariki na ukanda wa nchi za SADC.

6.11 Hali kadhalika, Mwenyekiti aliwajulisha wawekezaji kuwa katika mkutano wa Wenyeviti wa Bodi na Watendaji wa Taasisi jijini Arusha, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan, aliyaelekeza mashirika ya umma ambayo yana uwezo, kuendesha shughuli zake za kiuchumi na zenye kuleta faida kutoka nje ya Tanzania. UTT AMIS ikiwa katika utekelezaji wa Mpango Mkakati wake, inatarajia kuwafikia na kuwahudumia Wawekezaji wengi zaidi nchini Tanzania, Ukanda wa Afrika Mashariki na Ukanda wa nchi za SADC. Katika kutekeleza hilo, UTT AMIS imekuwa ikifuatilia maendeleo ya soko katika jumuiya hizo mbili kwa kipindi cha miaka kadhaa. Matokeo ya awali yanaonyesha kwamba baadhi ya nchi zina fursa nzuri. UTT AMIS itaimarisha na kuelekeza nguvu katika kuchambua masoko haya mapya ili kufanya maamuzi sahihi na kwa wakati muafaka. Ukizingatia lengo la Mkakati la kuongeza thamani ya Mifuko, ni muhimu kuwa kila fursa inayopatikana iweze kutumika vyema. Kwa kuzingatia kuwa ninyi Wawekezaji mnazifahamu faida za uwekezaji katika mifuko inayoanzishwa na kusimamiwa na UTT AMIS, Mwenyekiti aliwaomba Wawekezaji waendelee kuwa mabalozi wazuri juu ya uwekezaji kwa familia, marafiki, ndugu pamoja na jamaa zao.

6.12 Mwisho, Katika kuhitimisha taarifa yake, Mwenyekiti aliwashukuru wote kwa ushirikiano na imani yao kwa UTT AMIS na Mfuko wa Watoto kwa kipindi chote cha mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2024. Kwa namna ya kipekee aliishukuru Serikali kupitia Wizara ya Fedha, Ofisi ya Msajili wa Hazina, Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana, Msimamizi wa Mifuko ambaye ni Benki ya CRDB, Soko la Hisa la Dar es Salaam pamoja na Madalali wake, Wajumbe wenzake wa Bodi ya Wakurugenzi, Wafanyakazi wa UTT AMIS na Wadau wote ambao wameendelea kuiwezesha UTT AMIS kutekeleza majukumu yake katika mwaka huu wa fedha. Alieleza matumaini yake kuwa ushirikiano huu utaendelea kwa manufaa ya Wawekezaji na maendeleo ya Soko la Mitaji na Sekta ya Fedha hapa Nchini kwetu.

## 7.0 TAARIFA YA MWANGALIZI WA MFUKO

7.1 Mwakilishi wa Benki ya CRDB ambaye ni Mwangalizi wa Mfuko wa Watoto, aliwasilisha Taarifa iliyoeleza kwamba, kama waangalizi wa Mfuko wa Watoto, wana jukukumu la kusimamia na kuhakikisha kwamba utendaji wa meneja wa mfuko unaendana/ unazingatia waraka wa makubaliano ili kuhakikisha maslahi bora ya wenye vipande. Katika utekelezaji wa kazi hiyo, mwangalizi wa mfuko ana majukumu yafuatayo; Uangalizi wa mali za mfuko, kuhakikisha meneja wa mfuko anatumia njia/mbinu sahihi katika kukokotoa mahesabu ya thamani ya mfuko sambamba na mkataba wa makubaliano, na pia kuhakikisha viwango vya uwekezaji vinazingatiwa.

7.2 Mwakilishi huyo alieleza kuwa Katika kipindi cha mwaka wa fedha, kilichoanzia tarehe 01.07.2023 mpaka 30.06.2024, Benki ya CRDB kama mwangalizi wa mfuko wa Watoto, imeendeleza uangalizi wa mwenendo wa shughuli za meneja wa mfuko, utekelezaji wake na kuangalia changamoto kwenye uwekezaji.

7.3 Mwakilishi wa Benki ya CRDB alihitimisha kwa kuwathibitishia Wawekezaji wa Mfuko kwamba shughuli za uwekezaji kwenye mfuko wa Watoto na wajibu wa meneja wa mfuko (UTT AMIS), vimeendeshwa/ vimetekelezwa kufuatana na vipengele vya waraka wa makubaliano. Tukizingatia suala la imani/ uaminifu wa wenye vipande kwenye mfuko, tunathibitisha kwamba maslahi ya wenye vipande ndani ya mfuko wa Watoto yanalindwa na kuzingatiwa ipasavyo, na meneja ameendesha mfuko kulingana na waraka wa makubaliano.

## 8.0 TAARIFA YA MWAKA KUHUSU UKAGUZI WA HESABU ZA MFUKO WA WATOTO

8.1 Mwakilishi kutoka Shirika la Wahasibu la KPMG ambao ni Wakaguzi wa Mfuko aliwasilisha Muhtasari wa Taarifa kuhusu ukaguzi wa Hesabu za Mfuko kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2024. Alieleza kuwa Taarifa ya Hesabu za Mfuko zilizowasilishwa yaani Taarifa ya Mapato na Matumizi, Taarifa ya Urari wa Hesabu za Mfuko, Taarifa ya Mabadiliko ya Thamani ya Mfuko na Taarifa ya Mtiririko wa Fedha umetayarishwa kutoka katika taarifa kamili ya ukaguzi ya Mfuko wa Watoto kwa kipindi cha mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2024.

8.2 Taarifa ilieleza kuwa Muhtasari wa taarifa ya hesabu za fedha haioneshi taarifa zote kwa mujibu wa viwango vya kimataifa vya utoaji wa taarifa za kifedha (International Financial Reporting Standards (IFRS)). Taarifa ya wakaguzi iliendelea kusema Muhtasari huu wa hesabu pamoja na hii taarifa yetu siyo mbadala wa taarifa kamili ya hesabu za kifedha iliyokaguliwa. Muhtasari wa hesabu za kifedha pamoja na taarifa kamili ya hesabu zilizokaguliwa haijumuishi matukio au miamala baada ya tarehe za taarifa ya hesabu za fedha zilizokaguliwa.

8.3 Pia taarifa ilieleza kwamba maoni ya ukaguzi (audit opinion) yasiyokuwa na kasoro juu ya taarifa kamili ya ukaguzi wa hesabu za fedha za Mfuko yalitolewa kwenye taarifa ya tarehe 11 Novemba, 2024 kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2024. Taarifa kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2024 inajumuisha mambo mengine muhimu juu ya ukaguzi wa hesabu za Mfuko.

8.4 Mwakilishi huyo alihitimisha taarifa yake kwa kueleza kuwa majukumu yao kama wakaguzi wa hesabu za Mfuko ni kutoa maoni kama muhtasari wa hesabu za Mfuko unaendana na taarifa kamili ya ukaguzi wa hesabu za fedha na kwa mujibu wa taratibu zao za ukaguzi, ukaguzi ambao ulifanywa kwa mujibu wa viwango vya kimataifa vya ukaguzi (International Standards on Auditing–ISA) 810 (kama ilivyorekebishwa), kuhusu “Kazi za kuripoti juu ya Muhtasari wa taarifa za fedha”.

## 9.0 TAARIFA YA MWAKA KUHUSU HESABU ZA MFUKO WA WATOTO

Mkurugenzi wa Fedha na Mipango wa Kampuni ya Uwekezaji ya UTT AMIS aliwasilisha Taarifa ya Hesabu za Mfuko kwa kipindi cha mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2024.

9.1 Mkurugenzi aliwaomba wawekezaji kusoma taarifa kwa kulinganisha hali ya utendaji wa Mfuko kwa miaka miwili (2) iliyoishia mwezi Juni, 2024 na Juni 2023 na kwamba taarifa imegawanyika katika sehemu kuu nne, ambazo ni Taarifa ya Mapato na Matumizi (Statement of Profit or Loss and Other Comprehensive Income), Taarifa ya Urari wa Hesabu za Mfuko (Statement of Financial Position), Taarifa ya Mabadiliko ya Thamani ya Mfuko (Statement of Changes in Net Assets Attributable to Unit Holders) na Taarifa ya Mtiririko wa Fedha (Statement of Cash Flows).

9.2 Kwa upande wa Mapato na Matumizi, Taarifa ilieleza kuwa, katika kipindi cha mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2024, jumla ya Mapato ya Mfuko yalikuwa Shilingi 2,337,789,000 /= ikilinganishwa na Mapato ya Shilingi 1,164,048,000/= kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2023. Kuongezeka kwa mapato kunatokana na kuongezeka kwa viwango vya faida ya uwekezaji katika maeneo mbalimbali ya uwekezaji kutokana na mabadiliko ya soko. Pia ilielezwa kuwa jumla ya Gharama za Uendeshaji kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2024 zilikuwa Shilingi 387,578,000/= ikilinganishwa na Shilingi 206,028,000/= kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2023, hivyo kufanya Faida baada ya kutoa gharama za uendeshaji na kabla ya kodi kuwa Shilingi 1,950,211,000/= ikilinganishwa na Faida ya Shilingi 958,020,000/= mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2023. Kodi iliyotozwa na Serikali ilikuwa Shilingi 15,532,000/= ikilinganishwa na Shilingi 5,271,000/= kwa mwaka wa fedha 2023. Hivyo, Mfuko ulibaki na Faida Halisi (baada ya Kodi na Matumizi) ya Shilingi 1,934,679,000/= ikilinganishwa na Shilingi 952,749,000/= mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2023.

9.3 Kwa upande wa Urari wa Hesabu za Mfuko, ilielezwa kuwa, Rasilimali za Mfuko zilikuwa ni Shilingi 19,183,414,000/= mnamo tarehe 30 Juni, 2024, ikilinganishwa na Shilingi 11,029,354,000/= tarehe 30 Juni, 2023. Dhima za Mfuko zilikuwa na jumla ya Shilingi 185,047,000/= mnamo tarehe 30 Juni, 2024, ikilinganishwa na Shilingi 242,003,000/= tarehe 30 Juni, 2023. Kutokana na taarifa hiyo, thamani halisi ya Mfuko tarehe 30 Juni, 2024 ilikuwa ni Shilingi 18,998,367,000/= ikilinganishwa na Shilingi 10,787,351,000/= tarehe 30 Juni 2023.

9.4 Kwa upande wa Taarifa ya Mabadiliko ya Thamani ya Mfuko, thamani ya Mfuko Mwanzoni mwa Mwaka wa fedha ulioishia 30 Juni 2024 ilikuwa Shillingi 10,787,351,000/= ikilinganishwa na Shillingi 5,726,519,000/= mwanzoni mwa Mwaka wa fedha ulioishia 30 Juni 2023. Ongezeko kutokana na faida ya Mfuko kwa kipindi cha mwaka ulioishia Juni 2024 ilikuwa ni Shilingi 1,934,679,000/= ikilinganishwa na Shilingi 952,749,000/= kwa mwaka linganishi ulioishia tarehe 30 Juni, 2023. Kwa upande wa miamala ya wenye vipande, mfuko ulipokea (Net sales) kiasi cha Shillingi 6,276,337,000/= kwa mwaka

wa fedha ulioishia 30 Juni 2024 ikilinganishwa na kiasi cha Shilingi 4,108,083,000/= kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2023. Miamala hiyo imepelekea mabadiliko ya thamani halisi ya Mfuko kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2024, kuwa Shilingi 18,998,367,000/= ikilinganishwa na Shilingi 10,787,351,000/= kwa mwaka 2023.

9.5 Kwa upande wa Taarifa ya Mtiririko wa Fedha, ilielezwa kuwa fedha halisi iliyotokana na shughuli za uendeshaji kabla ya marekebisho ya mtaji kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2024, ilitumika Shilingi 370,294,000/= ikilinganishwa na Shilingi 77,471,000/= kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2023. Fedha halisi iliyotumika kutoka kwenye shughuli za Uendeshaji baada ya marekebisho ya mtaji na kodi ya Serikali ilikuwa Shilingi 5,091,281,000/= ikilinganishwa na Shilingi 3,976,544,000/= kwa mwaka wa fedha 2023. Miamala ya Amana kwa wawekezaji ilipatikana fedha kiasi cha shilingi 6,276,337,000/= tarehe 30 Juni, 2024 ikilinganishwa na fedha kiasi cha shilingi 4,108,083,000/= tarehe 30 Juni, 2023. Miamala hiyo ilipelekea kubaki na salio la fedha kiasi cha Shillingi 1,185,056,000/= mwaka wa fedha uliosha 30 Juni, 2024 ukilinganisha na Shillingi 131,539,000/= 30 Juni, 2023. Aidha Mfuko ulikuwa na akiba ya Fedha kiasi cha Shilingi 289,485,000/= mwanzoni mwa mwaka wa fedha 2024 ikilinganishwa na akiba ya Shilingi 157,946,000/= mwanzoni mwa Mwaka wa Fedha 2023, Mfuko umeweza kubaki na akiba ya fedha kiasi cha Shilingi 1,474,541,000/=, mwishoni mwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2024 ikilinganishwa na Shilingi 289,485,000/=, mwishoni mwa mwaka wa fedha wa 2023.

## 10.0 TAARIFA YA MENEJA WA MFUKO KUHUSU UWEKEZAJI

Mkurugenzi wa Idara ya Uendeshaji ya Kampuni ya Uwekezaji ya UTT AMIS aliwasilisha Taarifa ya Meneja kuhusu uwekezaji katika kipindi cha mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2024.

10.1 Taarifa ilieleza kuwa ukubwa wa Mfuko wa Watoto umeongezeka kwa Shilingi billioni 8.2 sawa na asilimia 76.6 kufikia billioni 18.9 ikilinganishwa na ongezeko la shillingi billioni 5.0 mwaka 2023. Thamani ya kipande imeongezeka kutoka shilingi 583.7 hadi kufikia shilingi 666.5 sawa na ongezeko la Shilingi 82.8 ikilinganishwa na ongezeko la Shilingi 64.4 kwa mwaka 2023.

10.2 Taarifa iliainisha mgawanyo wa uwekezaji wa Mfuko wa Watoto katika kipindi cha mwaka wa fedha ulioisha tarehe 30 Juni 2024, Kampuni ya UTT AMIS kama Meneja wa Mfuko alitumia uzoefu na weledi katika kufikia mgawanyo anuai wa Rasilimali kwa mujibu wa matakwa ya sera za mfuko wa Watoto. Taarifa ilieleza kuwa mgawanyo wa uwekezaji katika Mfuko wa Watoto uligawanyika katika asilimia kama ifuatavyo, asilimia 15.7 iliwekezwa katika Hisa, asilimia 77.6 iliwekezwa katika Dhamana za Serikali za muda mrefu, asilimia 6.7 katika Amana za benki za muda mfupi.

10.3 Faida ya Mfuko wa Watoto kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2024 ilikuwa asilimia 14.1 ikilinganishwa na asilimia 12.4 ya mwaka uliopita. Ilielezwa kuwa kuongezeka kwa kiwango cha faida ni kutokana na kuongezeka kwa viwango vya faida kwenye maeneo ya uwekezaji ikilinganishwa na hali ilivyokuwa mwaka uliopita. Mkurugenzi wa Uendeshaji aliendelea kusema hali na viwango vya faida iliongezeka kama inavyoonekana kwenye jedwali namba mbili (ii) kwenye taarifa ya meneja kuhusu uwekezaji.

10.4 Mkurugenzi aliwaeleza wawekezaji mambo mengine muhimu ya kuzingatia wakati wa kulinganisha faida za uwekezaji katika Mfuko wa Watoto pamoja na amana za benki, alieleza kuwa viwango vya riba za benki vilivyoonyeshwa ni kabla ya kutoa kodi ya zuio (withholding tax) ya asilimia 10 wakati mapato ya mfuko wa Watoto ni baada ya kutoa kodi ya zuio ya asilimia 10. Pia, jambo lingine la muhimu la kuzingatia ni kwamba mfuko wa Watoto unaruhusu wanachama wake kuuza vipande vyao wakati wowote hivyo kumpa fursa mwekezaji kupata fedha pindi anapozihitaji na kwamba hakuna kiwango cha chini cha uwekezaji kinachoruhusu kupata faida, viwango vya faida ya mfuko inatolewa sawa kwa wawekezaji wote (wawekezaji wa kipato kidogo, wa kipato cha kati na wale wenye kipato kikubwa).

10.5 Kuhusu pato la Taifa, Mkurugenzi alisema kuwa kwa mwaka 2023 uchumi ulikua kwa kiwango cha asilimia 5.1, ikilinganishwa na kiwango cha asilimia 4.7 mwaka 2022 (kama ilivyooneshwa kwenye jedwali III). Aidha, Kilimo, Ujenzi na Madini vilikuwa vichocheo vikubwa vya ukuaji wa uchumi katika kipindi hicho. Uchumi kwa mwaka 2024 unakadiriwa kuongezeka kwa asilimia 5.4, ukichagizwa na kufufuliwa kwa shughuli za kiuchumi hususani uwekezaji kwenye sekta ya umma na binafsi nchini. Mwasilishaji aliendelea kueleza kuwa, pato la taifa hutafasiri kiwango na shughuli za uchumi katika nchi. Hali imara na stahimilivu juu ya mwenendo wa uchumi nchini ni muhimu kwa Mifuko ya uwekezaji wa pamoja inayosimamiwa na UTT AMIS na maeneo mengine ya uwekezaji nchini. Uchumi imara husaidia kutunza na kuimarisha thamani ya uwekezaji na huvutia wawekezaji wa ndani na nje ya nchi.

10.6 Hali ya mfumuko wa bei nchini hadi kufikia tarehe 30 Juni 2024 ilikuwa asilimia 3.1 ikilinganishwa

na asilimia 3.6 iliyonakiliwa tarehe 30 Juni 2023. Kupungua kwa mfumuko wa bei nchini kunaashiria gharama za bidhaa na huduma mbalimbali zilipungua kwa mwaka ulioishia Juni 2024, ikilinganishwa na kasi iliyokuwepo Juni 2023. Hali ya uchumi nchini na mwenendo wa mfumuko wa bei ni stahimilivu kiasi ambacho kimewezesha wawekezaji kwenye mifuko ya uwekezaji kuwekeza kwa wingi. UTT AMIS inajitahidi kuwekeza kwenye maeneo yanayotoa faida shindani kuliko kiwango cha mfumuko wa bei.

10.7 Kuhusu Sekta ya benki, Mkurugenzi alieleza kuwa Kwa kipindi cha mwaka mmoja ulioisha tarehe 30 Juni, 2024 hali ya utendaji kwa sekta ya benki nchini imeendelea kuwa imara kwani jumla ya rasilimali na amana ziliongezeka. Asilimali ziliongezeka kutoka shilingi trilioni 53.7 iliyonakiliwa Juni 2023 hadi shilingi trilioni 62.0 Juni 2024. Kiasi cha amana kiliongezeka kwa shilingi trilioni 4.9 sawa na asilimia 13.7 kutoka shilingi trilioni 35.7 Juni 2023 hadi shilingi trilioni 40.6 Juni 2024. Jumla ya mikopo ilifikia shilingi trilioni 37.4 ikilinganishwa na shilingi trilioni 31.5 mwaka uliopita. Mifumo ya malipo kwa njia ya digitali nchini iliendelea kuwa imara, ikithibitishwa na kuwepo kwa kiwango cha juu cha miamala iliyokamilika kwa muda mfupi. Kwa mwaka 2023 idadi ya miamala iliyofanyika kutoka kwenye huduma za pesa mtandaoni Kwenda benki ni million 6.6 yeneye yenye thamani ya shilingi trilioni 2.7. Kwa kipindi hicho, idadi ya miamala iliongezeka kwa asilimia 34.1 na thamani yake ilikua kwa asilimia 25.2. Kuendelea kuimarika kwa sekta ya benki ni muhimu kwa mifuko ya uwekezaji wa pamoja na uchumi kwa ujumla kwani huduma zitolewazo na benki huchochea ufanisi kwenye uchumi. Aidha, hadi tarehe 30 Juni, 2024 meneja wa mifuko ya uwekezaji wa pamoja amefanikiwa kuunganisha mifumo ya UTT AMIS na benki ili kuwawezesha wawekezaji kununua vipande kidigitali, hivyo kurahisisha uwekezaji mahali popote.

10.8 Mkurugenzi alieleza namna sekta ya mawasiliano inavyoendelea kuchochea na kurahisisha Uwekezaji katika mifuko na huduma binafsi. Jumla ya mauzo ya vipande yaliopokelewa na UTT AMIS kupitia mitandao ya simu za mikononi ni shilingi bilioni 47.4 mwaka 2024 ikilinganishwa na shilingi bilioni 25.4 yaliopokelewa mwaka 2023. Taarifa iliainisha kuwa kwa kupiga *150*82# au kwa kutumia programu tumizi mwekezaji anaweza kufungua akaunti na kuanza Uwekezaji wake. Aidha kupitia simu mwekezaji anaweza kununua na kuuza vipande.

10.9 Kuhusu Dhamana za Serikali ilielezwa kuwa Kwa kipindi cha mwaka mmoja ulioisha tarehe 30 Juni, 2024, Benki Kuu ya Tanzania kwa niaba ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilipunguza kiasi cha dhamana za Serikali za muda mfupi sokoni kwa shilingi trilioni 0.6 hadi shilingi trilioni 2.7 Juni 2024. Hata hivyo, Uhitaji wa dhamana za Serikali za muda mfupi uliongezeka kwa shilingi trilioni 0.7 hadi kufikia shilingi trilioni 4.3 kutoka shilingi trilioni 3.6 mwaka jana. Aidha, kiasi kilichokubaliwa baada ya mnada kimeongezeka kwa asilimia 3.8 (shilingi trilioni 0.1) kutoka shilingi trilioni 2.5 hadi shilingi trilioni 2.6 Juni 2024. Kwa kipindi hicho, kiasi cha dhamana za Serikali za muda mrefu kilichouzwa kwenye soko la awali kilikuwa ni shilingi trilioni 3.3 ikilinganishwa na shilingi trilioni 4.3 mwaka uliopita. Kiwango cha ushiriki kwenye minada hiyo kiliongezeka hadi shilingi trilioni 5.2 (asilimia 11.5) ikilinganishwa na shilingi trilioni 4.6. Kiwango kilichokubaliwa na Benki Kuu ya Tanzania baada ya mnada kilipungua kwa shilingi trilioni 1.1 (asilimia 28.2) hadi shilingi trilioni 2.8 kikilinganishwa na shilingi trilioni 3.9 mwaka 2023. Kuongezeka kwa ushiriki na uwekezaji kwenye dhamana za Serikali kunaashiria ongezeko la uelewa kwa umma kuhusu uwekezaji na akiba. Ongezeko la uelewa na ushiriki katika soko la dhamana nchini husaidia kuboresha ukwasi na faida kweneye mifuko ya uwekezaji wa pamoja.

10.10 Kwa kipindi cha mwaka wa fedha kilichoishia Juni 2024, viwango vya riba zinazotolewa kwenye amana za benki hazikubadilika kwa kiwango kikikubwa. Wastani wa riba za mikopo ulikuwa asilimia 15.4 na riba kwa mkopo wa mwaka mmoja ni asilimia 15.8. Wastani wa faida kwa amana za benki ilikuwa asilimia 7.5 na faida kwa amana ya mwaka mmoja ilikuwa asilimia 8.7. Kiwango vya Riba katika dhamana za Serikali za muda mfupi ziliongezeka kutoka wastani wa asilima 6.5 mwezi Juni 2023 hadi kufikia asilimia 8.3 Juni 2024. Kiwango cha riba kwa mikopo ya siku kwa benki kilipanda hadi asilimia 7.2 kutoka asilimia 5.0 mwezi January 2024. Kamati ya sera ya fedha (MPC) ya Benki Kuu ilianza kutumia sera mpya ya fedha kwa kutumia mfumo wa riba ya benki kuu (CBR). Riba hiyo iliongezwa hadi asilimia 6.0 mwezi April 2024 kutoka asilimia 5.5 mwezi January 2024. Viwango vya faida kwa mwaka huu hususani kwenye dhamana za Serikali za muda mrefu ni zaidi ya viwango vilivyopatikana mwaka uliopita. Ongezeko la faida kwenye uwekezaji wa dhamana hizo huleta matokeo chanya kwenye faida kwa wawekezaji.

10.11 Kwa kipindi cha mwaka mmoja kilichoisha mwezi Juni 2024, Dola moja ya marekani iliuzwa shilingi 2,640 ikilinganishwa na shilingi 2,339.1 mnamo Juni 2023. Kwa kipindi cha mwaka mmoja Shilingi ya Tanzania ilishuka thamani kwa asilimia 12.8 ililinganishwa na asilimia 1.0 mwaka uliopita. Benki Kuu imechekua hatua kadhaa ikiwemo kuzuia utumiaji wa dola kwa mahitaji ya huduma na bidhaa zinazopatikana nchini. Hatua hizi zinatarajiwa kupunguza mahitaji ya fedha za kigeni, kuongeza akiba ya fedha za kigeni na kuimarisha thamani ya fedha ya Tanzania.

10.12 Aidha, ilielezwa kuwa ustahimilivu wa viwango vya kubadilisha fedha ni muhimu kwa mifuko ya uwekezaji wa pamoja ya UTT AMIS na Uchumi wa Tanzania kwa ujumla kwani husaidia kutunza thamani ya rasilimali ambazo thamani yake ipo katika shilingi za kitanzania. Kwa ujumla, Mifuko inayosimamiwa na UTT AMIS inatoa faida nzuri kwa Shilingi za Tanzania lakini inapobadilishwa hadi sarafu nyingine kama vile Shilingi ya Kenya au Dola ya Marekani faida inaweza kuathiriwa endapo kutakuwa na kupungua kwa thamani ya shilingi ya kitanzania katika kipindi hicho.

10.13 Kuhusu Soko la Mitaji na dhamana, taarifa ilieleza kuwa kwa kipindi cha mwaka mmoja kilichoishia Juni 2024, soko la mitaji na dhamana limekuwa imara na thabiti, kwani limepelekea kuongezeka kwa ushiriki wa wawekezaji katika soko la hisa, mitaji, dhamana na kwenye Mifuko ya Uwekezaji wa Pamoja. Soko limekuwa likifanya kazi vizuri kwa upande wa mauzo na shughuli mbalimbali.

Benki mbili za biashara ambazo ni CRDB na NMB ziliorodhesha hatifungani pamoja na hatifungani ya Mamlaka ya maji Tanga zenye thamani ya shilingi bilioni 482.4. Pia mifuko miwili ya uwekezaji wa Pamoja iliongezeka sokoni, ambayo ni Alpha Capital Ltd na Zan Securities Ltd. Hali ya ushiriki kwenye soko la mitaji, dhamana na uwekezaji kwenye mifuko ya pamoja nchini imeongezeka. Ni matarajio yetu kuwa hali hii itazidi kuimarika na kuongezeka zaidi. Kuingia kwa wasimamizi wapya wa mifuko ya uwekezaji wa Pamoja na fursa zingine za uwekezaji sokoni ni ishara nzuri kwa UTT AMIS na soko kwa ujumla. Tunatarajia Taasisi au kampuni zingine kujiunga ili kuongeza ukwasi na ushindani jambo ambalo litaongeza zaidi ufanisi, faida na huduma bora.

10.14 Taarifa ya Soko la Upili kwa dhamana na Hatifungani zilizoorodheshwa ilionyesha kuwa katika kipindi cha mwaka ulioishia Juni 2024, kiwango cha ushiriki kwenye eneo la dhamana za Serikali na Kampuni binafsi kimeongezeka licha ya faida kuwa ya wastani. Jumla ya dhamana za Serikali kupitia soko la upili imeongezeka kwa shilingi trilioni 0.6, sawa na ongezeko la asilimia 17.1, hadi shilingi trilioni 3.5 kutoka shilingi trilioni 2.9 mwaka uliopita. Jumla ya thamani za Hatifungani za Kampuni binafsi iliongezeka kwa shilingi bilioni 2.9, sawa na asilimia 74.4 kutoka shilingi bilioni 1.0 Juni 2023 hadi shilingi bilioni 3.9 mwaka huu. Ongezeko la thamani ya miamala limetokana na kuongezeka kwa hatifungani mpya zilizoorodheshwa sokoni.

10.15 Kuhusu Soko la Hisa, taarifa ilionyesha kuwa hali ya mauzo ya hisa na shughuli sokoni hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2024 ilikuwa ya kuridhisha. Thamani ya soko la Hisa la Dar es Salaam ilikuwa shillingi trilioni 16.8, ikwa juu kwa asilimia 12.0 kutoka shillingi trilioni 15.0 mwaka jana. Asilimia ya ushiriki kwa wawekezaji wa ndani ni wastani wa asilimia 76.2, ikilinganishwa na asilimia 69.6 mwaka 2023. Pia, Fahirisi ya Hisa kwa kampuni za ndani (TSI), iliongezeka kwa asilimia 9.3 hadi kufikia alama 4,475.2. Fahirisi ya Kampuni zote sokoni (DSEI) iliongezeka kwa asilimia 12.0 hadi kufikia 2,016.9. Jumla ya mauzo ya soko katika kipindi hicho, iliongezeka kwa shilingi bilioni 165.0 hadi shilingi bilioni 272.6 kutoka shilingi bilioni 107.6 mwaka uliopita. Katika kipindi hicho, baadhi ya Kampuni zilitangaza na kulipa gawio kwa wanahisa. Gawio lililolipwa kwa kila hisa lilikuwa kama ifuatavyo; TCC - Sigara (Tsh. 500.0), TWIGA (TPCC) (Tsh. 390.0), TBL (Tsh. 537.0), NMB (Tsh. 361.18), SWISS (Tsh. 51.33), VODA (Tsh. 9.95), DSE (Tsh. 145.0) na CRDB (Tsh. 50.0). Hivyo basi, kwa wawekezaji wote waliowekeza kwenye Kampuni tajwa hapo juu walipata gawio sawa na maelezo hapo juu.

10.16 Taarifa ya Mifuko ya Uwekezaji wa Pamoja, taarifa ilionyesha kuwa hadi tarehe 30 Juni, 2024 jumla ya rasilimali kwenye mifuko ya uwekezaji wa pamoja inayosimamiwa na Taasisi ya UTT AMIS ziliongezeka kwa shilingi bilioni 702.8 ikilinganishwa na ongezeko la shilingi bilioni 538.9 lililonakiliwa mwaka jana kutoka shilingi bilioni 1,550.7 hadi kufikia shilingi bilioni 2,273.6. Mabadiliko chanya katika jumla ya rasilimali yanaonesha kuongezeka kwa imani ya wawekezaji katika bidhaa za UTT AMIS kutokana na usalama, faida shindani na urahisi wa kuingia na kutoka kwenye uwekezaji.

10.17 Mkurugenzi alimalizia kwa kuwahakikishia wawekezaji wake kuwa UTTAMIS itaendelea kubuni na kuvumbua mianya na fursa za uwekezaji kadiri inavyojitokeza katika soko ili kuongeza mapato na faida kwa wawekezaji. Lengo likiwa ni kuvuka matarajio ya wawekezaji kwa maendeleo yao na Taifa kwa ujumla.

## 11.0 MASWALI MAONI NA MAJIBU

### 11.1 Wekezaji waliuliza maswali Pamoja na kutoa hoja zifuatazo:

11.1.1 Mwekezaji alitaka kujua kuhusu jitihada zinazofanyika kuwafikia kwenye kutoa elimu kwa Watoto ilikusaidia Watoto kukua na elimu ya uwekezaji.

11.1.2 Mwekezaji alitoa maoni, kuhusu umuhimu wa mzazi kupata nafasi ya kutoa fedha kwa mwaka mara moja ili kuongeza chachu ya wazazi kuwekaza zaidi katika huu mfuko na pia waweze kupata nafasi ya kulipa ada.

11.1.3 Mwekezaji alitoa mapendekezo ya kuwepo kwa bima katika mfuko wa Watoto au kuanzisha mfuko ili kusaidia Watoto pindi wakiwa wanaumwa.

11.1.4 Pongezi nyingi zilitolewa kwa Meza kuu na Mwenyekiti wa bodi, pia mwekezaji alitoa ushauri wa kutoa mabegi ya shule kwa Watoto yenye nembo ya UTT AMIS ili kuvutia Watoto wengi kujiunga na UTT AMIS na kuja kwenye mkutano wa Mfuko wa Watoto. Zaidi aliongezea kwa kuomba kuboreshwa kwa mifuko ya AGM ili kuleta mvuto mzuri kwa kutumika mtani na watu kupata kuijua na kujiunga zaidi UTT AMIS.

11.1.5 Mwekezaji alitoa mapendekezo juu ya kuwepo kwa darasa la uwekezaji kwa Watoto kabla ya kuanza kwa mkutano.

11.1.6 Mwekezaji aliomba kufahamu juu ya mapato mengineo na maelekezo zaidi kuhusiana na kushuka kwa mapato husika.

11.1.7 Mwekezaji alitoa mapendekezo kuhusu uwepo wa darasa la zoom kwenye kutoa elimu ili kuwafikia watu wengi hasa wale wanaoshidwa kufika kwenye vituo vya kutoa huduma.

11.1.8 Mwekezaji aliuliza ni kwanini akaunti za Watoto huandikishwa kwa jina la mzazi badala la mtoto.

11.1.9 Mwekezaji aliomba kufahamu kuhusu uhusiano wa kati ya mauzo ya vipande na gharama ya vipande.

11.1.10 Mwekezaji alitaka kujua mchakato wa kupata haki zake pale ambapo mzazi atakapokuwa kafariki.

11.1.11 Mwekezaji alitoa maoni ya kuanzishwa kwa UTT Foundation itakayosaidia katika tafiti mbalimbali na misaada ambayo italeta faida kwa kupata ajira, kusaidia jamii na kukuza mfuko.

### 11.2 Wawakilishi wa Kampuni ya Uwekezaji ya UTT AMIS walitoa ufafanuzi na Majibu ya maswali kama ifuatavyo:

11.2.1 Kuhusu jitihada zinazofanyika kuwafikia Watoto wengi zaidi kwa ajili ya kuwekeza, ilijibiwa kuwa jitihada kubwa zimefanyika kuwafikia wazazi na Watoto ili kuwekeza katika mfuko huu na mfuko umekua ikilinganishwa na mwaka wa fedha uliopita kwa ongezeko kubwa. Jitihada zaidi zitaendelea kufanyika ili kuweza kuwafikia wazazi na Watoto kwa wingi zaidi.

11.2.2 Kuhusu kutoa fedha kwenye mfuko wa Watoto japo kwa mwaka mara moja, Wawekezaji walitolewa wasiwasi na kuelezwa kwamba iliwekwa kutoa fedha mpaka mtoto kufikia miaka 12 kwa sababu iliaminika kwamba ndio muda mtoto anaenda kusoma shule zinazotumia fedha nyingi, lakini kama mwekezaji anauhitaji mkubwa wa kutoa fedha anaruhusiwa ila kutakuwa na mchakato wa idhini.

11.2.3 Kuhusu uwepo wa Bima kupitia mfuko wa Watoto, mwakilishi alieleza kwamba limechukuliwa na litaangaliwa namna bora nzuri zaidi ya kulifanyia kazi.

11.2.4 Maoni ya muwekezaji kuhusu kupewa mabegi kwa Watoto na kuboreshwa kwa mifuko ya wawekezaji yalichukuliwa na Mkurugenzi aliahidi utendaji wake kuanzia mwaka ujao.

11.2.5 Kuhusu uwepo wa darasa la uwekezaji kwa Watoto kabla ya mkutano wa Mfuko wa Watoto, ilielezwa kuwa linachukuliwa na maboresho yatafanyika kwa kuangalia namna sahihi ya utekelezaji wake.

11.2.6 Ufafanuzi ulitolewa kuwa, mapato mengineyo ni mapato yanayotokana na fedha zinazotolewa na meneja kulipia matumizi yaliyozidi kiwango cha matumizi ya mfuko kama ilivyo elezwa kwenye waraka wa makubaliano na mapato kutokana na hati fungani zilizouzwa kwa faida ili kuwekeza kwenye fursa nzuri zaidi. Kuhusu kushuka kwa mapato hayo, inatokana na kutokuuza kwa hati fungani mwaka husika na kupelekea kutokea na chazo kimoja cha mapato mengineyo ambacho ni malipo yaliolipwa na meneja kwa matumizi yaliyozidi kiwango cha waraka wa makubaliano ukilinganisha na mwaka uliopita.

11.2.7 Kuhusiana na mikutano au madarasa ya zoom, ilielezwa kuwa madarasa hayo yapo na yanafanyika ila siyo kwa kutumia zoom, ilielezwa kuwa maoni hayo yamepokelewa kwa nia ya kuboresha zaidi na kuweka utaratibu mzuri kwa kuchagua siku katika wiki, mwezi au robo mwaka ili wawekezaji na wawekezaji watarajiwa waweze kujiunga na kushiriki na zaidi kupata elimu ya

uwekezaji ya UTT AMIS.

11.2.8 Ilielezwa kuwa sababu ya akaunti ya mtoto kuwa na jina la mzazi ni za kisheria kwanza, kwa kuwa mtoto hawezi kuingia katika mikataba yeye mwenyewe, ni lazima kuwe na mtu mzima ambaye ni mwangalizi (guarantor). Pia, kiuendeshaji, inasaidia katika kufikisha taarifa mbalimbali kama za mikutano. Hata hivyo, maboresho yatafanyika ili jina la juu liwe la mtoto likifuatiwa na la mlezi au mzazi.

11.2.9 Ufafanuzi ulitolewa juu ya uhusiano wa mauzo ya vipande na gharama ya mauzo ya vipande, ilielezwa kuwa ni vitu viwili vyenye mausiano ila siyo wa moja kwa moja. Mauzo ya vipande ni fedha ambazo wawekezaji wanazileta kwa ajili ya uwekezaji na gharama ya mauzo ya vipande ni gharama ambazo meneja anazitumia kufikisha fedha kwa wawekezaji mfano gharama za miamala. Gharama hizi zimeongezeka kwa sababu miamala mwaka huu wa fedha ni mingi ukulinganisha na mwaka uliopita.

11.2.10 Ilielezwa kuwa kwa taratibu zilizokuwepo kila akaunti huwa na mrithi aliyeorodheshwa kwa maana hiyo atakuja na utambulisho na baada ya kujiridhisha, uwekezaji utahamishwa kwenye akaunti ya uwekezaji wake, ila ikitokea hakukuwa na mrithi aliyeorodheshwa, taratibu za kimahakama zitafuatwa.

11.2.11 Kuhusu kufunguliwa kwa UTT Foundation, ilielezwa kuwa kwa sasa UTT AMIS inatoa huduma kwa jamii kwa kiasi, siyo kwa ukubwa sana ila kadri Taasisi itakavyokuwa kubwa zaidi tukafikia mahala na kuweza kutoa angalau 1% ya faida inayopatikana basi menejimenti itaangalia namna ya kulifanyia kazi.

## 8.0 KUFUNGA MKUTANO

Baada ya kipindi cha Maoni, Maswali na Majibu, Mwenyekiti aliwashukuru Wawekezaji wote kwa kuhudhuria katika Mkutano huo. Pia aliwahakikishia kuwa mawazo na mapendekezo yaliyotolewa katika Mkutano huu yatazingatiwa na yale yanayowezekana yatatekelezwa. Mwisho aliwatakia heri ya sikukuu za Krismasi na Mwaka Mpya 2025. Mkutano ulifungwa saa kumi na moja na dakika kumi (11:10) jioni.

................................ ................................

**MWENYEKITI** **KATIBU**

................................

**TAREHE**

Watoto Fund
Faraja kwa Watoto

# KIAMBATISHO “A”

## ORODHA YA WAWEKEZAJI WA MFUKO WA WATOTO WALIOHUDHURIA KWENYE MKUTANO WA KUMI NA MBILI (12) WA MWAKA WA MFUKO ULIOFANYIKA KATIKA UKUMBI WA MIKUTANO WA KITUO CHA MIKUTANO CHA KIMATAIFA CHA JULIUS NYERERE, DAR ES SALAAM TAREHE 17 NOVEMBA 2024

| S/NO | JINA LA MWEKEZAJI |
|---|---|
| 1 | ABDALLAH OMARI IDOWA |
| 2 | ABDALLAH OMARI IDOWA |
| 3 | ABDULRAHIM ALLY BARUANI |
| 4 | ABEDI MBANOTI TUMOI |
| 5 | ABUBAKARI JABU NYUNDO |
| 6 | ADAM MUSA MUKAMA |
| 7 | ADELINA SOSTHENES KARUGABA |
| 8 | AHMED ABUBAKAR MZEE |
| 9 | AHMED MOHAMED ZEIN |
| 10 | AHMED MOHAMED ZEIN |
| 11 | AHOBOKILE DUNCAN MAJILLAH |
| 12 | AKIDA RAMADHANI MWAIMU |
| 13 | AKIDA RAMADHANI MWAIMU |
| 14 | AKONGO MASOUD HASSAN |
| 15 | ALBANO MICHAEL MAHECHA |
| 16 | ALFRED GERALD MSACKY |
| 17 | ALLEN ALFRED MOLLEL |
| 18 | ALLY ISMAIL MUNIS |
| 19 | ALOISIA ISDORY MUSHI |
| 20 | ALOISIA MARY LEKULE |
| 21 | ALOISIA MARY LEKULE |
| 22 | AMANYILE ZABRON MAHALI |
| 23 | AMOS MICHAEL NGAILO |
| 24 | ANDREW OTHNIEL NAMINGA |
| 25 | ANDREW OTHNIEL NAMINGA |
| 26 | ANESTUS GASTO RUTAKANGWA |
| 27 | ANGANILE BERNARD KALINGA |
| 28 | ANGEL RAPHAEL MAPUNDA |
| 29 | ANITHA FREDRICK MWIJAGE |
| 30 | ANNA JONASAI MAPHOLE |
| 31 | ANNA KISIMBI VICENT |
| 32 | ANNA LUCAS NYUMBA |
| 33 | ANNA NAFTAL KAWICHE |
| 34 | ANNA NAFTAL KAWICHE |
| 35 | ANNAH ABRAHAM MUSHALA |
| 36 | ANNAH JAMES LUSEKELO |
| 37 | ANSELMA CASMIR KULAYA |
| 38 | ANTHONY AMINI MASSAWE |
| 39 | ANTIGONI SAADAM LUDOVICK |
| 40 | ASANTE ERICK HYERA |
| 41 | ASSELA PONTIAN DOMITIAN |
| 42 | ASSINA ABDALLAH HASSAN |
| 43 | ATHANAS GIDEON CHIHWALO |
| 44 | ATHUMANI MAULID SHABAN |
| 45 | AUGUST BENEDICT KOWERO |
| 46 | BAHATI ANDREW MWANYINGILI |
| 47 | BAHATI WILLISON NYAMSAKI |
| 48 | BARAKA NASRI MWAMPETA |
| 49 | BARAKA NASRI MWAMPETA |
| 50 | BARAKA NASRI MWAMPETA |
| 51 | BARAKA PAULO CHARLES |
| 52 | BARBAS MATHIAS IGOGO |
| 53 | BEATH GULABAGANILA CHRISTOPHER |
| 54 | BEATRICE FREDRICK TERUGWA |
| 55 | BEATRICE FREDRICK TERUGWA |
| 56 | BENEDICTO RENATUS RAPHAEL |
| 57 | BENJAMIN PAUL MUNG’ARWE |
| 58 | BICHI HUSSEIN BRUNO |
| 59 | BICHI HUSSEIN BRUNO |
| 60 | BICHI HUSSEIN BRUNO |
| 61 | BICHI HUSSEIN BRUNO |
| 62 | BLANCA PIUS MASSAWE |
| 63 | BLANDINA EMMANUEL MNYAGA |
| 64 | BLANDINA EMMANUEL MNYAGA |
| 65 | BRENDA JOSHUA KILEO |
| 66 | BRIAN KULWA MOSHI |
| 67 | BULIGA MUJAGA SWEMA |
| 68 | BUPE AMOS SIJANGA |
| 69 | BUPE AMOS SIJANGA |
| 70 | CATHERINE ELIBARIKI MUSHI |
| 71 | CATHERINE VINCENT MASSENGA |
| 72 | CHARLES MICHAEL KAHUNGU |
| 73 | CHARLES THOBIAS MADOVA |
| 74 | CHARLES THOBIAS MADOVA |
| 75 | CHEYO PAULO NKELEGE |
| 76 | CHOLA NAMBEYA RUPIA (Rep. Chola Rupia) |
| 77 | CHRISTINA CASTOR LYARI |
| 78 | CHRISTINA CASTOR LYARI |

| | |
|---|---|
| 79 | ISTINA GEORGE MALUGANJE (Rep. Christina Geor |
| 80 | CHRISTINA JOSEPH KABADI |
| 81 | CHRISTINA JOSEPH KABADI |
| 82 | CHRISTINA SAMWEL CHUNGA |
| 83 | CHRISTINA SIMON MISANA |
| 84 | CHRISTOPHER LAWRANCE KANNONYELE |
| 85 | CLEMENTINA CHIFULE MANASSEH |
| 86 | CONSTANSIA RICHARD MGENI |
| 87 | DAMARY WILSON MACHUME |
| 88 | DANFORD DEOGRATIAS RUGAZIA |
| 89 | DANIEL GODFREY MANDARI |
| 90 | DANIEL RICHARD HUMBLE |
| 91 | DAYAN REUBEN OLEKUNEY |
| 92 | DENIS DAVID ZIDADI |
| 93 | DENIS LIBERATUS MAGGESA |
| 94 | DENIS SHUKURU KAIZA |
| 95 | DEOKRASIAS FEDRICK KIMARIO |
| 96 | DESIDERY KAKWEZI ATHANAS |
| 97 | DIANA CHARLES LUKONDO |
| 98 | DOMINA JOSEPHATH MONGI |
| 99 | DOMINA JOSEPHATH MONGI |
| 100 | DOROTHY STEPHEN BIKURAKULE |
| 101 | DOSTEUS MTINDE LOPA |
| 102 | EDDA DAUDI KONDELA |
| 103 | EDMUND MWOMBEKI NKUBA |
| 104 | EDSON ENOCK KIKULI |
| 105 | ELIA JACOB HASSANI |
| 106 | ELIA NELSON MTWEVE |
| 107 | ELIAKIMU MTWALE MAMBILE |
| 108 | ELIYA REGNALD MTWEVE |
| 109 | ELIZABETH ERNEST LYIMO |
| 110 | ELIZABETH FREDRICK OWOYA |
| 111 | EMILIE SHABANI MSUYA |
| 112 | EMMANUEL AZZORY MARWA |
| 113 | EMMANUEL ELIMWOKOZI KIMEA |
| 114 | EMMANUEL ELIMWOKOZI KIMEI |
| 115 | EMMANUEL JOSEPH KASANGA |
| 116 | EMMANUEL JOSEPH KASANGA |
| 117 | EMMY ADRIAN TEMBA |
| 118 | ERIC MAHENDEKA MUGURUSI |
| 119 | ERICK PRIMMY KILENGA |
| 120 | ERNEST PHELICIAN SHIRIMA |
| 121 | ESTHER PHABIAN KATAMBI |
| 122 | EUNICE SAIMON MLACKY |
| 123 | EUNICE SAIMON MLAKI |
| 124 | EUNICE THEOPHIL KANZA |
| 125 | EVA ISIDORY MASSAWE |
| 126 | EVALIN YOHANA MSENGI |
| 127 | EVALIN YOHANA MSENGI |
| 128 | EVANS AMOS MSHUMBUSI |
| 129 | EVANS AMOS MSHUMBUSI |
| 130 | EVELYN JOHN CHIWANGO |
| 131 | EVELYN JOHN CHIWANGO |
| 132 | RA ELIA NYAMLUNDWA (Rep. Ezra Elia Nyamlundw) |
| 133 | FARAJA CHARLES MGAYA |
| 134 | FARAJI NURU KOTI |
| 135 | FATUMA MOHAMED MAHUMBI |
| 136 | FATUMA SHABANI SIKA |
| 137 | FELEFU DOMU MAGAKA |
| 138 | FELISTINA FESTO KIPAO |
| 139 | FIDELIS BUDELELE YOMBYA |
| 140 | FIRDAWS SWALEH KOMBO |
| 141 | FLAVIA DAMAS KWAI |
| 142 | FLAVIA DAMAS KWAI |
| 143 | FLAVIA DAMAS KWAI (Rep. Fadhili O Kivyiro) |
| 144 | FLORENCE GODWIN ULEDI |
| 145 | FRANCIKAISE FRANCE MAGODA |
| 146 | FRANCIS PROCHES KITANGE |
| 147 | FRANCKAISE FRANK MAGODA |
| 148 | FRANK BENADI SAIMONI |
| 149 | FRANK ENEA YESAYA |
| 150 | FRANK FIDAS LEMA |
| 151 | FRANK GILBERT BAKENGESA |
| 152 | FRANK YOSIA YONA |
| 153 | FRAVIA DAMAS KWAI (Rep. Noel Damas Kwai) |
| 154 | FREDRICK ERNEST GUNGAYENA |
| 155 | FREDRICK ERNEST GUNGAYENA |
| 156 | FREDRICK PASTORY MBOGO |
| 157 | GABRIEL AMIRI DAPU |
| 158 | GABRIEL AMIRI NDAPU |
| 159 | GASATI SILLA BHOKE |
| 160 | GEOFREY ABRAHAM SILUMBU |
| 161 | GEORGE CLEOPA MAPUNJO |
| 162 | GEORGE CLEOPA MAPUNJO MPEMBENI |
| 163 | GEORGE MARKI BINDE |
| 164 | GEORGE PHILIPO KOYAGE |
| 165 | GERALD VICTOR NGUYA |
| 166 | GERALD VICTOR NGUYA |
| 167 | GERRADY WILLIAM NAGHENDA |
| 168 | GERSHON JOHNSON MAZINGO |
| 169 | GETRUDA ROMAN MOSHA |
| 170 | GHUHEN REUBEN MTAITA |

| | |
|---|---|
| 171 | GHUHEN REUBEN MTAITA |
| 172 | GILBERT MUTAINDUKA GRATIAN |
| 173 | GLORIA GASPER MULAMULA |
| 174 | GLORIA LESHABARI MUSHI |
| 175 | GLORIA THOMAS MTEI |
| 176 | GLORY CUTHBERT NDOSSI |
| 177 | GODWIN ERNEST MATHEW |
| 178 | GODWIN ERNEST MATHEW |
| 179 | GODWIN ERNEST MELAY |
| 180 | GODWIN GABRIEL RWAKIBARILA |
| 181 | GODWIN MAGAFU KALYANYAMA |
| 182 | GOODLUCK BAKAR MCHOMVU |
| 183 | GRACE MAMNGODO MAZENGO |
| 184 | GRACE NYAKWESI BISWALO |
| 185 | GWAKISA ANANIA MWAMBUNGU |
| 186 | HADIJA ISMAIL SWALEHE |
| 187 | HADIJA WAZIRI MOHAMEDI |
| 188 | HALIMA RAJABU MONDO |
| 189 | HASHIM ABDUL KWEYAMBA |
| 190 | HASHIMU RAMADHANI MUSHI |
| 191 | HAWA SALIM MAUMBA |
| 192 | HELLEN ASTARIKO NYAHONGO |
| 193 | HERMAN KASHO LWAMBUGWE |
| 194 | HIDAN OMARY RICCO |
| 195 | HIDAYA ABDALLAH BUNGARA |
| 196 | HIDAYA KAMBI RASHID |
| 197 | HILDA AMOS KUBOJA |
| 198 | HILDA NICHORAUS MKALA |
| 199 | HOSSEN IDDI KAYUMBA |
| 200 | HUSSEIN BAKARI NDALI |
| 201 | IDDER SCUDDER ALFRED MSACKY |
| 202 | INNOCENT THOMAS PACHO |
| 203 | INNOCENT THOMAS PACHO |
| 204 | ISACK KELEMANI NYAKIHA |
| 205 | ISDORY CYPRIAN FITWANGILE |
| 206 | ISSA MOHAMED WAHICHINEDA |
| 207 | JACKQULINE JACKSON KALES |
| 208 | JACKQULINE JACKSON KALES |
| 209 | JACKQULINE JACKSON KALES |
| 210 | JACQUELINE AMANI ITATIRO |
| 211 | JACQUELINE JAMES NDUGULILE |
| 212 | JAMES AKONAAY AMO |
| 213 | JAMES KATABARO KAROKOLA |
| 214 | JANET SAMWEL KIVUYO |
| 215 | JANETH ATHANAS NYAMBALYA |
| 216 | JANETH PETER SHUNULA |
| 217 | JAPHET ALEX METHA |
| 218 | JAPHET ALEX METHA |
| 219 | JAPHET RAZIEL NYAMBO |
| 220 | JAPHET RAZIEL NYAMBO |
| 221 | JEHOVANUS STEPHEN SUMAYE |
| 222 | JERFASIA ATHANASI MFILINGE |
| 223 | JERFASIA ATHANASI MFILINGE |
| 224 | JERINI ANTHONY HOTTI |
| 225 | JESCA WANZITA PAUL |
| 226 | JESSICA ERNEST SWAI |
| 227 | JESSICA ERNEST SWAI |
| 228 | JESSICA ERNEST SWAI |
| 229 | JOEL SULEIMAN WAKINDA |
| 230 | JOHNY IBRAHIM ENOCK MWAKATOBE |
| 231 | JOSEPH ANDLEA MGAKA |
| 232 | JOSEPH GODFREY TARIMO |
| 233 | JOSEPH GODFREY TARIMO |
| 234 | JOSEPH IBRAHIM MWASONGWE |
| 235 | JOSEPH JULIUS KAZIMILI |
| 236 | JOSEPH LEONARD KASONGO |
| 237 | JOSEPH LUSSUNGU MDEJA |
| 238 | JOSEPHINE FRANCIS KAYUNGILIZI |
| 239 | JOSEPHINE LAURENT SIMON |
| 240 | JOSHUA ELLY NZIKU |
| 241 | JOVIN SEBASTIAN SIMBA |
| 242 | JOYCE ANNE MILLINGA |
| 243 | JOYCE EDWARD MWAKALUKWA |
| 244 | JULIETH JEREMIA MACHA |
| 245 | JULIUS JIMM MLWAFU |
| 246 | JULIUS SEBASTIAN MTWEVE |
| 247 | JULIUS SEBASTIAN MTWEVE |
| 248 | JUMA BAKARI MUSSA |
| 249 | JUMA HUSSEIN KIAZE |
| 250 | KASIMU ABDALAH UGAMA |
| 251 | KATARINA CHRISTOPHER JOSEPH |
| 252 | KATARINA CHRISTOPHER JOSEPH |
| 253 | KELVIN ALOYCE KINYAGA |
| 254 | KISICHOFAA MOHAMED KILENGA |
| 255 | KOKUWAISA JOSEPH GONDO |
| 256 | KOMBO ABDALLAH LUWANJA |
| 257 | KOMBO ABDALLAH LUWANJA |
| 258 | KULOLA NATHANAEL MANDAGO |
| 259 | KULWA DEOGRATIUS DOLLAR |
| 260 | LEMAH JOHNSTONE MWAITUKA |
| 261 | LEOCADIA CHAZUA MKUMBI |
| 262 | LEOCADIA PANTALEO NJAU |
| 263 | LEONARD FUNGAMTAMA LUKONGOLA |
| 264 | LIBERATOR BENEDICT MSIGWA |

| | |
|---|---|
| 265 | LILIAN APPOLINARY NYAMBIBO |
| 266 | LILIAN ISKARI NYENYE |
| 267 | LILIAN ISKARI NYENYE |
| 268 | LILIAN KOKUSHERULA NYOMBI |
| 269 | LILLIAN REUBEN MAHERI |
| 270 | LINDA JOSEPH RUJWEKA |
| 271 | LOVE EDWARD NATHANIEL |
| 272 | LOYCE MAGESA MWITA |
| 273 | LUCIA ALDO LIKASI |
| 274 | LUCY THADEUS MALLYA |
| 275 | LUCY THADEUS MALLYA |
| 276 | LUCY THADEUS MALLYA |
| 277 | LYDIA LAZARO NYIRENDA |
| 278 | LYISON THOMAS KALULUNGA |
| 279 | MAKALANGA NESTORY MSABILA |
| 280 | MARIA ALFONCE MGULUNDE |
| 281 | MARIA JOSEPHINA GODA |
| 282 | MARIAM HAMIDU MAWA |
| 283 | MARIAM HAMIDU MLAWA |
| 284 | MARIAM MOHAMED KIMOLO |
| 285 | MARIAM MOHAMED KIMOLO |
| 286 | MARIAM SHABANI MWAGIZE |
| 287 | MARIAMMASOUD MAHUGU |
| 288 | MARIAPIA PIUS NGEZE |
| 289 | MARY ATHANASIO MWAMASIMBI |
| 290 | MARY GEORGE MIHAMBO |
| 291 | MARY KASSIAN SHAURITANGA |
| 292 | MARY OSMUND KIPENGELE |
| 293 | MARY PASCAL MABITI |
| 294 | MARYAM MASHAKA FAUSTINE |
| 295 | MARYAM MASHAKA FAUSTINE |
| 296 | MARYAM MASHAKA MUGANZI |
| 297 | MARYAM MUHIDDIN SALUM |
| 298 | MATHIAS GODFREY KAVISHE |
| 299 | MATILDA GEOFFREY RUSIBAMAJILA |
| 300 | MAUREEN CHISOTE KABOPOLE |
| 301 | MICHAEL JOSEPH CHOPELO |
| 302 | MIRIAM PHINIAS MCHUNGA |
| 303 | MKAMI WEBIRO MASIGITI |
| 304 | MOHAMED MUSSA NGONYE |
| 305 | MOHAMED SELEMANI NASSORO |
| 306 | MOSES IBRAHIM NGAUGULA |
| 307 | MOSES RAMADHAN KAMWEKA |
| 308 | MSEI LOISHIYE MOLLEL |
| 309 | MVUMO AARON BALATI |
| 310 | MWADHANI SAIDI KUMBILAMOTO |
| 311 | MWANAMVUA HASSAN ALMASSY |

| | |
|---|---|
| 312 | MWITA BERNARD MEGABE |
| 313 | NAISHIJA LOISHIYE SAIBULL |
| 314 | NAMSI IBRAHIM HUSSEIN |
| 315 | NAOMI WINFARESS MUNUO |
| 316 | NASRA HABIBU ALLY |
| 317 | EMA LEONARD MAANGA (Rep. Clinton Prosper Sw |
| 318 | NEEMA SAMWEL SASSI |
| 319 | NEEMA TITUS MUSHI |
| 320 | NICODEMOS DOMINICK LEKEI |
| 321 | NICODEMOS DOMINICK LEKETI |
| 322 | NONOSIUS SIMON MBIGI |
| 323 | NURU IKUPA MWASAMPETA |
| 324 | NURU IKUPA MWASAMPETA |
| 325 | NYANJURA REUBEN NYARUGA |
| 326 | OLIMPIA JOHN FREDRICK |
| 327 | OMARY ABDULRAHMANI MUHANI |
| 328 | OMARY HAMIS KAUKUYA |
| 329 | OWEN THEMISTOCLES RWEBANGIRA |
| 330 | PASKAZIA RWEGASIRA NTINABO |
| 331 | PATIENCE BENWARD NDUNGURU |
| 332 | PAUL JACKSON MWAIKENDA |
| 333 | PAUL JACKSON MWAIKENDA |
| 334 | PAUL MALEHIWA NHIGULA |
| 335 | PAVAN JAYANT VAGHELA |
| 336 | PENDO JOACHIM KIOMBWE |
| 337 | PHYLLICY JAMES PUNJIKA |
| 338 | PRISCA OTMARY HAULE |
| 339 | PRISCA STAMBULI KISELA |
| 340 | PROSPER JOSEPH SAKAYA |
| 341 | PROSPER ELIASON BILACHA |
| 342 | RAFAELI SAMWELI MLAHAGWA |
| 343 | RAHAB NJERI WANGAI |
| 344 | RAHIMA NURDIN DOSSA |
| 345 | RASHOSE NELSON MAWALA |
| 346 | RASHOSE NELSON MAWALA |
| 347 | RAVASCO SONDAS MWAKISU |
| 348 | REBEKA JANKE KILIMA |
| 349 | REHEMA A MDEMU |
| 350 | REHEMA A MDEMU |
| 351 | REHEMA A MDEMU |
| 352 | REHEMA EMILIUS FUSI |
| 353 | REHEMA EMILIUS FUSI |
| 354 | REHEMA SALUM DIBEGA |
| 355 | REHEMA SALUM DIBEGA |
| 356 | RENATUS ANTHONY MALAWA |
| 357 | RICHARD CHARLES CHACHA |

| | |
|---|---|
| 358 | RODAVELA SOSTHENES NDETABULA |
| 359 | ROGATHE EDUMAELI URASSA |
| 360 | ROMANUS OKUNGU ROMANUS |
| 361 | ROSE BLUCHARD KABENGULA |
| 362 | ROSEMARY NIYO BGOYA |
| 363 | ROSEMARY NIYO BGOYA |
| 364 | ROY CHRISTOPHER FOYA |
| 365 | SAID MOHAMED KIBAO |
| 366 | SAIMON JOHN MWIMI |
| 367 | SAIMON JOHN MWIMI |
| 368 | SALAMA MOHAMED WAZIRI |
| 369 | ALAMA TWAHIR MARIJANI (Rep. Ismail Abbas Kilun) |
| 370 | SALOME AGRIPA SENKA |
| 371 | SALOME FRANK MTIBILI |
| 372 | SALOME MOPHATE GESOGWE |
| 373 | SALOME SAMSON MPALI |
| 374 | SALOME SAMSON MPALI |
| 375 | SAMSON CLEMENT MDUNDU |
| 376 | SARA ERASTO KWEKA |
| 377 | SARAPHINA ANDREW TIBAMBALA |
| 378 | SARAPHINA ANDREW TIBAMBALA |
| 379 | SAUDA ALLY MKANULA |
| 380 | SAUMU AMIRI MPOLE |
| 381 | SELVA SEBASTIAN MAJALIWA |
| 382 | SHANGWE YUDA KASIMBA |
| 383 | SHOSE HENRY MAKULE |
| 384 | SIFA BADI SHEKALAGHE |
| 385 | SOFIA PASKAL BANGUZE |
| 386 | SOPHIA GEOFFREY MGAYA |
| 387 | SOPHIA GEOFFREY MGAYA |
| 388 | SOPHIA MOHAMED MBAJO |
| 389 | SOPHIA RICHARD MGAYA |
| 390 | STELLA SAMWEL AYENGO |
| 391 | STEVEN DUSTAN MAPUNDA |
| 392 | SUBIRA ISSAYA MWAKALINDILE |
| 393 | SULEIMAN WAKINDA JOSEL |
| 394 | SUZAN HABAKUKI MZIRAY |
| 395 | SUZANA MELKIOR MBWAGAI |
| 396 | SYLVANUS ALFRED NTIRUMOLEKWA |
| 397 | SYLVIA INNOCENT NJOVU |
| 398 | SYLVIA INNOCENT NJOVU |
| 399 | TABU OMARY MSOVU |
| 400 | THADEO MATHEO SAKULA |
| 401 | THERESIA KABULA RENATUS |
| 402 | THERESIA SALVATORY MGUMBA |
| 403 | THOMAS JOACHIM MMASSY |

| | |
|---|---|
| 404 | TIMOTHY KAJINA OBALA |
| 405 | TULI GALLEN MWAKYUSA |
| 406 | TULI GALLEN MWAKYUSA |
| 407 | TULI MWAKYUSA MWAIPAJA |
| 408 | TULIZO PATRICK KIBASA |
| 409 | TUMAINI STEPHEN MIKAPAGARO |
| 410 | TWAHA ATHUMAN MTHIMKHULU |
| 411 | TWAHA BAKARI JUMBE |
| 412 | TWILUMBA DICKSON MAKENE |
| 413 | TWILUMBA DICKSON MAKENE |
| 414 | TWILUMBA MAKENE |
| 415 | TWILUMBA MAKENE |
| 416 | VALERIAN FAUSTIN PETER |
| 417 | VENANCE MPWEHUKA NYUGU (Rep. Ve) |
| 418 | VENERANDA BERNARD MSEMWA |
| 419 | VERONICA ARNOLD MISANA |
| 420 | VERONICA MARIA RWEGASIRA |
| 421 | VERONIKA KASANDA SHIJA |
| 422 | VICTOR MAGABE MAGAMBO |
| 423 | VIOLET MATUKI MAHERI |
| 424 | VIOLETH ROBERT SHAYO |
| 425 | VIOLETH ROBERT SHAYO |
| 426 | VIOLETH ROBRT SHAYO |
| 427 | VUPE URSULA LIGATE |
| 428 | WAILES EZEKIEL MWASHAMBWA |
| 429 | WAILES EZEKIEL MWASHAMBWA |
| 430 | WALTER ELISA KIMARO |
| 431 | WALTER ELISA KIMARO |
| 432 | WAZIRI HASSANI KARATA |
| 433 | WILBAFOS JULIUS KIRUMBA |
| 434 | WILBAFOS JULIUS KIRUMBA |
| 435 | WILBAFOS JULIUS KIRUMBA |
| 436 | WILSON JOHN NKUZI |
| 437 | WINFRIDA ELIAB CHIDUO |
| 438 | WINFRIDA RICHARD SOLLY |
| 439 | WINNIE EFATHA KITALI |
| 440 | YANDE BERNADETHA PANYA |
| 441 | YANDE BERNADETHA PANYA |
| 442 | YANDE BERNADETHA PANYA |
| 443 | YASINTA JULIUS MTUGA |
| 444 | YUSTINA HENRICK MASANYONI |
| 445 | ZAHARA MIRAJI SIMBA |
| 446 | ZAINA HENRY CHONJO |
| 447 | UNI MOHAMED SALIMU (Rep. Ayman Andrew Eman) |
| 448 | ITUNI MOHAMED SALIMU (Rep. Azhar Hamisi Shaba) |

Watoto Fund Faraja kwa Watoto

| | |
|---|---|
| 449 | ZAWAJUDI SAID MAKENE |
| 450 | NYAKIMURA ELIAS MUHOJI |
| 451 | OMARY HAMIS KAUKUYA |
| 452 | BEATUS JOHN KILAWE |
| 453 | SAUMU AMIRI MPOLE |
| 454 | LILLIAN REUBEN MAHERI |
| 455 | CHACHA MARWA ISSAROW |
| 456 | FRANK YOSIA YONA |
| 457 | RODNEY OBADIAH ALANANGA |
| 458 | IBRAHIM MUSSA LUTHER |
| 459 | NICODEMOS DOMINICK LEKEI |
| 460 | SHOSE HENRY MAKULE |

Watoto Fund
Faraja kwa Watoto

# 3 Yatokanayo na Mkutano Mkuu wa Kumi na Moja

Hakukuwa na yatokanayo na Mkutano Mkuu uliopita wa Mfuko wa Watoto


Watoto Fund
Faraja kwa Watoto

# TAARIFA FUPI YA MWAKA YA MFUKO WA WATOTO

# 4 Barua ya Mwenyekiti wa Bodi

# BARUA YA MWENYEKITI KWA WAWEKEZAJI WA MFUKO WA WATOTO KWA MWAKA 2025

**Ndugu Wawekezaji,**



Kwa niaba ya Bodi ya Wakurugenzi, ninayo furaha kuwakaribisha nyote katika Mkutano Mkuu wa Kumi na Tatu (13) wa Mfuko wa Watoto Tunawashukuru kwa kutenga muda wa kuhudhuria mkutano huu ambao utajadili maendeleo ya Mfuko kwa mwaka wa fedha ulioishia 30 Juni 2025.

Ndugu wawekezaji, nina imani mmekuwa mkifuatilia maendeleo ya Mfuko na kwamba mmeipokea, kuipitia na kuichambua taarifa ya Mfuko kwa kipindi cha mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2025. Ninayo furaha kuwajulisha kuwa utendaji wa mfuko kwa kipindi hicho umeendelea kuwa mzuri na wakuvutia. Faida kwa wawekezaji ilikuwa kubwa ikilinganishwa na kigezo linganifu (performance Benchmark). Faida kwa mwaka ilikuwa asilimia 15.8 ikilinganishwa na asilimia 14.1 ya mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2024. Faida iliyopatikana imeenda sambamba na maendeleo ya soko la fedha na ni kubwa kuliko kigezo linganifu cha asilimia 12.1. Katika kipindi cha mwaka wa fedha ulioishia Juni 2025, thamani ya mfuko iliongezeka kutoka Shilingi bilioni 19.0 iliyofikiwa tarehe 30 Juni 2024 hadi Shilingi bilioni 31.5 tarehe 30 Juni 2025. Ongezeko la thamani ya Mfuko limetokana na faida nzuri iliyopatikana pamoja na kuongezeka kwa uelewa juu ya faida zinazopatikana katika Mifuko ya uwekezaji wa pamoja.

## Mwenendo wa Uchumi na Mazingira katika Soko la Fedha

Ndugu wawekezaji, kwa mujibu wa Ofisi ya Taifa ya Takwimu, hali ya uchumi nchini Tanzania imeendelea kuimarika. Pato la Taifa (Gross Domestic Product) lilikua kwa asilimia 5.5 kwa mwaka 2024 na inategemea kukua kwa asilimia 6.0 kwa mwaka 2025. Kiwango hiki cha ukuaji uchumi unaifanya nchi ya Tanzania kuwa miongoni mwa nchi za Afrika Mashariki na za Ukanda wa Ushirikiano wa Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) ambazo Uchumi wake unakua vizuri. Kwa mujibu wa taarifa za Benki Kuu ya Tanzania, mfumuko wa bei ulikuwa kati ya asilimia 3.0 hadi 3.3 kwa kipindi kilichoishia tarehe 30 June 2025 ikilinganishwa na matarajio ya kiwango cha kati ya asilimia 3.0 hadi 5.0. Kiwango hiki pia kimeendana na matarajio ya nchi za ukanda wa Afrika Mashariki cha asilimia 8.0 na kiwango cha kati ya asilimia 3.0 hadi 7.0 kwa nchi za SADC. Kwa kipindi cha mwaka mmoja ulioishia tarehe 30 Juni 2025, viwango vya riba katika soko havikubadilika sana na hivyo kuashiria utulivu wa soko kwa ujumla. Kwa upande mwingine, thamani ya shilingi ya Tanzania dhidi ya dola ya Marekani ilibaki kuwa imara ambapo iliimarika kwa kiwango kidogo cha asilimia 0.3.

Kuhusu maendeleo ya Soko la Mitaji na Dhamana, maendeleo mazuri yameshuhudiwa katika kipindi cha mwaka ulioishia tarehe 30 June 2025. Mtaji katika soko la hisa la Dar es Salaam umeongezeka kwa asilimia 16.7 kutoka kiasi cha shilingi trillioni 16.8 tarehe 30 June 2024 hadi trilioni 19.6 tarehe 30 Juni 2025. Pia, bei ya Hisa zilizoorodheshwa zimeongezeka kama inavyo onyeshwa na Fahirisi (Tanzania Share Index). Katika kipindi cha mwaka kilichoishia tarehe 30 Juni 2025, kumekuwa na ongezeko la Fahirisi la asilimia 8.4 ambapo iliongezeka toka 4,475.20 tarehe 30 Juni 2024 hadi 4,852.30 tarehe 30 Juni 2025. Hali hii inaonyesha kwamba, katika kipindi cha mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2025, bei za hiza kwa ujumla ziliongezeka. Sababu za kupanda kwa bei za Hisa kulichagizwa na kufanya vyema kwa Makampuni yaliyoorodheshwa katika Soko la Hisa la Dar es Salaam na kuongezeka kwa imani ya wawekezaji wa ndani na nje ya nchi na kuboreshwa kwa mazingira ya biashara na uwekezaji hapa nchini. Tunaishukuru Serikali kwa ujumla kwa kuendelea kuweka mazingira bora ya biashara na usimamizi nchini.

## Utendaji wa Mifuko na Maendeleo Mengineyo

Ndugu Wawekezaji, kuhusu utendaji wa Mifuko kwa mwaka wa fedha unaoishia 30 Juni 2025, viashiria vya kiuchumi vinaonyesha kwamba, Kampuni ya UTT AMIS pamoja na Mifuko inayoisimamia imeendelea kufanya vizuri. Thamani ya Mifuko imeongezeka kutoka Shilingi Trilioni 2.2382 tarehe 30 Juni 2024 hadi kufikia Shilingi Trilioni 3.2687 tarehe 30 Juni 2025. Hili ni ongezeko la shilingi 1.0305 trilion sawa na asilimia 46.0 ikilinganishwa na ongezeko la shilingi bilioni 702.8, sawa na asilimia 45.7 kwa mwaka uliotangulia. Ongezeko la ukubwa wa Mifuko limetokana na ongezeko la idadi ya Wawekezaji 143,990, sawa na asilimia 44.0 waliojiunga katika Mfuko kwa mwaka 2025 ikilinganishwa na Wawekezaji 79,519, sawa na asilimia 32.0 waliojiunga mwaka wa fedha uliotangulia. Kama nilivyosema hapo awali kwamba mifuko yote imetoa faida nzuri kwa wawekezaji wake.

Ndugu Wawekezaji, katika kipindi cha mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2025, Kampuni ya UTT AMIS iliendelea na utekelezaji wa Mpango Mkakati mpya wa miaka mitano. Awali, Mpango huu ulipangwa kuhitimishwa katika mwaka wa fedha unaoishia Juni 30, 2029 lakini baadae ulifanyiwa marejeo na sasa utakamilika mwezi Juni, 2030 ili kuendana na mpango wa Serikali. Katika Mpango Mkakati Mpya, Kampuni ya UTT AMIS inatarajia kukuza uwekezaji katika Mifuko kutoka Trilion 2.2 mnamo tarehe 30 June 2024 mpaka Shilingi Trilioni 8.5 tarehe 30 June 2030. Zaidi ya hapo, miongoni mwa malengo ya taasisi ni pamoja na kuendelea kutoa huduma za kidijitari huku ikiongeza idadi ya vituo vya huduma kwa wateja ili kusogeza zaidi huduma kwa wawekezaji. Kama ambavyo mmeshuhudia, UTT AMIS imekamilisha maboresho ya Mfumo wa kisasa wa kutolea huduma. Mfumo huu utaruhusu uchakataji wa miamala mingi zaidi kwa wakati, kupatikana kwa huduma mbalimbali na hivyo wawekezaji kufurahia huduma zitolewazo na UTT AMIS. Kampuni ya UTT AMIS itaendelea kuuelimisha umma juu ya huduma za kidijitali zinazopatikana katika mfumo mpya.

## Matarajio ya mwaka wa fedha 2025/2026

Ndugu Wawekezaji, kwa kipindi cha mwaka wa kwanza wa utekelezaji wa Mpango Mkakati wa UTT AMIS unaoiishia Juni 2030 umewezezesha thamani ya mifuko kufikia Shilingi trilioni 3.27 ukilinganisha na matarajio ya ukuaji wa hadi trilioni 2.79. Ukuaji huu unatoa msingi wa kuyafikia malengo ya thamani ya mifuko. Kwa kuzingatia mageuzi ambayo kampuni ya UTT AMIS inayatekeleza, maendeleo ya sasa katika soko na mazingira bora ya biashara ambayo yamefanywa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, nimatumaini yetu kuwa mifuko itaendelea kutoa faida nzuri kwa wawekezaji huku ikiendelea na uboreshaji wa uendeshaji na utoaji huduma kwa wateja ili kusaidia juhudi za ukuzaji wa mitaji kwa wawekezaji.

## Dira ya Maendeleo 2050

Kama mnavyokumbuka, tarehe 17 Julai 2025, Tanzania ilizindua Dira ya Maendeleo ya miaka 25 hadi 2050 yenye lengo mahsusi la kukuza pato la Nchi kutoka Dola za Kimarekani Bilioni 85 za sasa hadi Dola Trilioni Moja kiasi ambacho ni takribani mara kumi na mbili. Njia mojawapo ya kuweza kufikia lengo hilo ndani ya kipindi cha miaka ishirini na tano ijayo ni kuendelea kuwekeza akiba yako katika mifuko ya UTT AMIS. Nipende kukuhakikishia kuwa uwekezaji wa UTT AMIS unafanywa kwa weledi na wataalamu wetu katika maeneo ambayo ni salama na yenye tija chini ya usimamizi wa Bodi ya Wakurugenzi na Mamlaka za usimamizi za Umma kama vile Mamlaka ya Usimamizi wa Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA) na Benki Kuu ya Tanzania. Kama Mwekezaji, umefanya uamuzi sahihi wa kuwekeza katika mifuko ya Uwekezaji wa pamoja kama vile Mfuko wa **Watoto.** Uamuzi huo ni njia nzuri ya kutawanya fedha zako katika uwekezaji anuai huku ukifurahia maajabu ya Kampaundi. Hii itakufanya uendelee kupata faida ukiwa umelala au unaendelea na shughuli nyingine. Aidha, inatupasa kuzingatia ushauri wa aliyekuwa Mfanyabiashara Maarufu marehemu billionea Charlie Munger, ya kwamba "Usikatize uwekezaji wako bila ya kulazimika kufanya hivyo" kwa maneno mengine, utanufaika na maajabu ya Kampaundi endapo uwekezaji wako utakaa kwa muda mrefu pasipo kuuza vipande vyako. Hii ni mojawapo ya njia ya uhakika ya kujitengenezea utajiri endelevu kwa manufaa yako binafsi na kwa jamii na hivyo kushiriki kikamilifu katika kusaidia taifa kulifikia lengo la pato la Dola za Kimarekani trilioni moja.

## Shukrani

Ndugu Wawekezaji, Kwa kuhitimisha, napenda niwashukuru nyote kwa ushirikiano na imani yenu kwa UTT AMIS na Mfuko wa Watoto kwa kipindi chote cha mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2025. Kwa namna ya kipekee nipende kuishukuru Serikali kupitia Wizara ya Fedha,Ofisi ya Msajili wa Hazina, Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana, Msimamizi wa Mifuko ambaye ni Benki ya CRDB, Soko la Hisa la Dar es Salaam pamoja na Madalali wake, Wajumbe wenzangu wa Bodi ya Wakurugenzi, Wafanyakazi wa UTT AMIS na Wadau wote ambao wameendelea kuiwezesha UTT AMIS kutekeleza majukumu yake katika mwaka huu wa fedha. Ni matumaini yangu kuwa ushirikiano huu utaendelea kwa manufaa ya Wawekezaji wetu na maendeleo ya Soko la Mitaji na Sekta ya Fedha hapa Nchini kwetu.

Prof. Faustin Rweshabura Kamuzora
**Mwenyekiti wa Bodi**

# 5 Taarifa ya Mwangalizi wa Mfuko wa Watoto

**CRDB BANK PLC**
Makao Makuu: Barabara ya Ally Hassan
Mwinyi / Barack Obama
S.L.P. 268, Dar es Salaam - Tanzania
Simu: +255 (0) 22 211 7441-7
Nukushi: +255 (0) 22 211 6714
Barua pepe: info@crdbbank.co.tz
Tovuti: www.crdbbank.co.tz

# TAARIFA YA MWANGALIZI WA MFUKO WA WATOTO KWA WAWEKEZAJI

Tukiwa ni waangalizi wa Mfuko wa **Watoto**, Jukumu letu ni kusimamia kwamba utendaji wa meneja wa mfuko unaendana/ unazingatia waraka wa makubaliano ili kuhakikisha maslahi bora ya wenye vipande. Katika utekelezaji wa kazi hii, mwangalizi wa mfuko ana majukumu yafuatayo; Uangalizi wa mali za mfuko, kuhakikisha meneja wa mfuko anatumia njia/mbinu sahihi katika kukokotoa mahesabu ya thamani ya mfuko sambamba na mkataba wa makubaliano, na pia kuhakikisha viwango vya uwekezaji vinazingatiwa.

Katika kipindi cha mwaka huu wa fedha, kilichoanzia tarehe 01.07.2024 mpaka 30.06.2025, Benki ya CRDB kama mwangalizi wa mfuko wa **Watoto**, tumeendeleza uangalizi wa mwenendo wa shughuli za meneja wa mfuko, utekelezaji wake na kuangalia changamoto kwenye uwekezaji.

Kwa kuzingatia hayo, tunapenda kuwathibitishia kwamba shughuli za uwekezaji kwenye mfuko wa **Watoto** na wajibu wa meneja wa mfuko (UTT AMIS), vimeendeshwa/ vimetekelezwa kufuatana na vipengele vya waraka wa makubaliano. Tukizingatia suala la imani/ uaminifu wa wenye vipande kwenye mfuko, tunathibitisha kwamba maslahi ya wenye vipande ndani ya mfuko wa **Watoto** yanalindwa na kuzingatiwa ipasavyo, na meneja ameendesha mfuko kulingana na waraka wa makubaliano.

*Abdulmajid M. Nsekela*

**Afisa Mtendaji Mkuu na Mkurugenzi Mtendaji**

**Tarehe:** Novemba, 2025

# 6 Taarifa ya Mkaguzi wa Hesabu za Mfuko

# TAARIFA YA MKAGUZI KUHUSU MUHTASARI WA HESABU ZA MFUKO WA WATOTO (WATOTO FUND)

KPMG

Jengo la Luminary

Ghorofa ya 2, Kitalu Na. 574

Barabara ya Haile Selassie, Msasani

S. L. P 1160, Dar es Salaam

Simu: +255 22 2600330

Barua Pepe: info@kpmg.co.tz

Tovuti: www.kpmg.co.tz

### *Maoni*

Muhtasari wa hesabu za Mfuko ambao unajumuisha muhtasari wa Urari wa hesabu za Mfuko mnamo tarehe 30 Juni 2025, muhtasari wa Mapato na Matumizi, muhtasari wa Mabadiliko ya Thamani ya Mfuko pamoja na muhtasari wa Mtiririko wa Fedha umetayarishwa kutoka katika taarifa kamili ya ukaguzi ya Mfuko wa Watoto kwa kipindi cha mwaka unaoishia tarehe 30 Juni 2025.

Kwa Maoni yetu, Muhtasari wa Hesabu za Mfuko wa Watoto unaendana na taarifa kamili za hesabu za Mfuko zilizokaguliwa kulingana na vigezo vilivyoelezwa kwenye dokezo namba 1.

### *Muhtasari wa Taarifa ya Hesabu za Fedha*

Muhtasari wa taarifa ya hesabu za fedha haioneshi taarifa zote kwa mujibu wa viwango vya kimataifa vya utoaji wa taarifa za kifedha kama ilivyotolewa na Bodi ya Kimataifa ya usimamizi wa viwango vya utoaji taarifa za fedha (International Accounting Standard Board (IFRS Accounting Standards)). Muhtasari huu wa hesabu pamoja na hii taarifa yetu siyo mbadala wa taarifa kamili ya hesabu za kifedha iliyokaguliwa. Muhtasari wa hesabu za kifedha pamoja na taarifa kamili ya hesabu zilizokaguliwa haijumuishi matukio au miamala baada ya tarehe za taarifa ya hesabu za fedha zilizokaguliwa.

### *Taarifa ya Ukaguzi na Hesabu za Fedha zilizokaguliwa*

Maoni ya ukaguzi (audit opinion) yasiyokuwa na kasoro juu ya taarifa kamili ya ukaguzi wa hesabu za fedha za Mfuko yalitolewa kwenye taarifa ya tarehe  20 Novemba 2025 kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni 2025.

Taarifa kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni 2025 inajumuisha mambo mengine Muhimu juu ya ukaguzi wa hesabu za mfuko.

### *Majukumu ya Meneja Kuhusu Muhtasari wa Hesabu za Fedha za Mfuko*

Meneja wa Mfuko anahusika na utayarishwaji wa muhtasari wa hesabu za fedha za Mfuko kwa mujibu wa vigezo kama ilivyoainishwa kwenye dokezo namba 1.

### *Majukumu ya Mkaguzi wa Hesabu za Mfuko*

Majukumu yetu kama wakaguzi wa hesabu za Mfuko ni kutoa maoni kama muhtasari wa hesabu za Mfuko unaendana na taarifa kamili ya ukaguzi wa hesabu za fedha na kwa mujibu wa taratibu zetu za ukaguzi, ukaguzi ambao ulifanywa kwa mujibu wa viwango vya kimataifa vya ukaguzi (International Standards on Auditing-ISA) 810 (kama ilivyorekebishwa), “Kazi za kuripoti juu ya Muhtasari wa taarifa za kifedha”

**Hili ni toleo lililotafsiriwa la ripoti ya Mkaguzi liyosainiwa katika toleo la Kiingereza.**

## Dokezo Namba 1

### Dokezo juu ya vigezo vya kutayarisha Muhtasari wa Hesabu

Muhtasari wa taarifa ya hesabu za fedha umetayarishwa kutoka kwenye taarifa kamili ya ukaguzi, iliyotayarishwa kwa mujibu wa viwango vya kimataifa vya utoaji wa taarifa za kifedha (IFRS) mnamo tarehe 30 Juni 2025.

Taratibu za kutayarisha muhtasari wa hesabu za fedha unaitaka menejimenti kuamua kiwango cha taarifa zitakazojumuishwa katika muhtasari ili kuendana kwa kiwango kikubwa na taarifa kamili ya ukaguzi au kutoa taswira ya muhtasari iliyosawa na taarifa ya hesabu za fedha zilizo kaguliwa.

Menejiment imetayarisha hesabu hizi kwa kuzingatia vigezo vifuatavyo:

(a) Muhtasari wa Hesabu unajumuisha hesabu zote za mfuko zilizoko katika taarifa ya hesabu zilizokaguliwa;

(b) Taarifa zilizopo kwenye muhtasari wa hesabu zinashabihiana na taarifa ya hesabu za mfuko zilizokaguliwa na

(c) Jumla kuu, jumla ndogo pamoja na taarifa linganifu zilizopo kwenye hesabu zilizokaguliwa zimeonyeshwa pia katika muhtasari wa hesabu ulioandaliwa

Taarifa ya hesabu za mfuko wa Watoto zilizokaguliwa zinapatikana katika ofisi ya Kampuni ya Uwekezaji ya UTT (UTT AMIS).

# 7 Taarifa ya Hesabu za Mfuko

## TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI (Profit or Loss and Other Comprehensive Income) KWA MWAKA UNAOISHIA 30 JUNI 2025

| | 2025<br>TSH '000 | 2024<br>TSH '000 |
|---|---|---|
| Mapato yatokanayo na riba | 3,115,971 | 1,791,710 |
| Faida/(hasara) itokayo na mabadiliko ya thamani ya hisa na Dhamana | 360,584 | 528,795 |
| Mapato mengineyo | 850,238 | 17,284 |
| **Jumla ya Mapato** | **4,326,793** | **2,337,789** |
| Gharama za Meneja | (367,759) | (222,176) |
| Gharama za Mwangalizi wa Mfuko | (24,517) | (14,812) |
| Gharama za Ukaguzi wa Hesabu | (2,071) | (1,740) |
| Gharama za Matangazo | (40,117) | (23,085) |
| Gharama za Mauzo ya Dhamana na Hisa | (11,570) | (13,980) |
| Gharama za Mauzo ya Vipande | (178,224) | (108,584) |
| Gharama Za Ushauri | (967) | (1,443) |
| Gharama nyinginezo za Uendeshaji | (5,785) | (1,758) |
| **Jumla ya Gharama za Uendeshaji** | **(631,010)** | **(387,578)** |
| **Ongezeko la Thamani (Mapato) Kwa wawekezaji kabla ya Kodi** | **3,695,783** | **1,950,211** |
| Kodi ya Zuio | (45,772) | (15,532) |
| **Ongezeko la Thamani (Mapato) Kwa wawekezaji Baada ya Kodi** | **3,650,011** | **1,934,679** |
| Mapato mengineyo(other comprehensive income) | - | - |
| **Ongezeko halisi la thamani ya Mfuko** | **3,650,011** | **1,934,679** |

Watoto Fund

## URARI WA HESABU ZA MFUKO (BALANCE SHEET) MNAMO TAREHE 30 JUNI 2025

| | 2025<br>TSH '000 | 2024<br>TSH '000 |
|---|---|---|
| **Rasilimali za Mfuko** | | |
| Fedha Taslim | 146,936 | 1,474,541 |
| Amana za muda Maalum katika Mabenki | 5,741,230 | - |
| Dhamana za Serikali | 22,537,315 | 14,679,717 |
| Hisa | 3,253,726 | 2,987,145 |
| Rasilimali nyinginezo (other receivable) | 37,916 | 42,011 |
| **Jumla ya Rasilimali** | **31,717,123** | **19,183,414** |
| | | |
| **Dhima ya Mfuko** | | |
| Dhima Nyinginezo | (214,298) | (185,047) |
| **Jumla ya Dhima ya Mfuko** | **(214,298)** | **(185,047)** |
| | | |
| **Thamani Halisi ya Mfuko** | **31,502,825** | **18,998,367** |
| | | |
| **Inawakilishwa na:** | | |
| Thamani Halisi ya Mfuko | **31,502,825** | **18,998,367** |
| Idadi ya Vipande | 40,828,109 | 28,523,046 |
| **Thamani ya Kipande** | **771.60** | **666.07** |

# TAARIFA YA MABADILIKO YA THAMANI YA MFUKO (STATEMENT OF CHANGES IN NET ASSETS ATTRIBUTABLE TO UNIT HOLDERS) KWA MWAKA ULIOSHIA 30 JUNI 2025

| | 2025<br>TSH '000 | 2024<br>TSH '000 |
|---|---|---|
| **Thamani ya mfuko mwanzoni mwa mwaka(Julai 1)** | **18,998,367** | **10,787,351** |
| Mabadiliko/Ongezeko ya thamani ya mfuko | 3,650,011 | 1,934,679 |
| | **22,648,378** | **12,722,030** |
| **Miamala (Transactions) ya wenye vipande kwa mwaka** | | |
| Mauzo ya vipande (Sales) | 10,492,136 | 7,114,943 |
| Ununuzi ya vipande (Repurchase) | (1,637,689) | (838,606) |
| **Mabadiliko ya thamani ya mfuko** | **8,854,447** | **6,276,337** |
| **Thamani halisi ya Mfuko** | **31,502,825** | **18,998,367** |

Watoto Fund
Faraja kwa Watoto

# TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA (CASH FLOW STATEMENT) KWA MWAKA UNAOISHIA 30 JUNI 2025

| | 2025<br>TSH '000 | 2024<br>TSH '000 |
|---|---|---|
| **FEDHA ITOKANAYO NA SHUGHULI ZA UENDESHAJI** | | |
| Mapato baada ya Kodi | 3,650,011 | 1,934,679 |
| **Imerekebishwa na:** | | |
| Faida/(Hasara) itokanayo na mabadiliko ya thamani ya dhamana isiyostahili kugawana | (360,584) | (528,795) |
| Pato la gawio la hisa | (222,027) | (144,707) |
| Pato la riba | (2,893,944) | (1,647,003) |
| Gharama za Kodi | 45,772 | 15,532 |
| **Faida kabla ya mabadiliko ya Mtaji wa uendeshaji:** | **219,228** | **(370,294)** |
| **Mabadiliko ya Mtaji wa uendeshaji** | | |
| Kuongezeka / Kupungua kwa Amana katika Mabenki | (5,673,400) | - |
| Kuongezeka / Kupungua kwa Dhamana za Serikali | (8,537,912) | (5,923,325) |
| Uwekezaji katika Hisa | 94,003 | (857,908) |
| Ongezeko /(Kupungua) kwa rasilimali nyinginezo | 4,095 | (18,907) |
| Ongezeko /(Kupungua) kwa Dhima nyinginezo | 29,251 | (56,956) |
| | **(14,083,963)** | **(6,857,096)** |
| **Fedha iliyopatikana kutoka kwenye shughuli za uendeshaji** | **(13,864,735)** | **(7,227,390)** |
| Gawio iliyopokelewa | 222,027 | 144,706 |
| Riba iliyopokelewa kutoka kwenye Dhamana | 3,226,113 | 2,006,935 |
| Riba iliyopokelewa kutoka kwenye Amana za Mabenki | 280,315 | - |
| Kodi iliyolipwa | (45,772) | (15,532) |
| **Fedha halisi (iliyotumika)/itokanayo na shughuli za uendeshaji** | **(10,182,052)** | **(5,091,281)** |
| **AMANA YA MFUKO (FINANCING ACTIVITIES)** | | |
| Mauzo ya Vipande (Sales of Units) | 10,492,136 | 7,114,943 |
| Ununuzi (Repurchase) wa Vipande | (1,637,689) | (838,606) |
| **Fedha halisi iliyopatikana/(iliyotumika) kutokana na miamala ya wenye vipande** | **8,854,447** | **6,276,337** |
| **Ongezeko halisi la Fedha** | **(1,327,605)** | **1,185,056** |
| **Salio la fedha mwanzoni mwa Mwaka** | **1,474,541** | **289,485** |
| **Salio la fedha mwishoni mwa Mwaka** | **146,936** | **1,474,541** |

.....................................
**Mwenyekiti wa Bodi**
**Tarehe:** Novemba, 2025

.....................................
**Mkurugenzi**
**Tarehe:** Novemba, 2025

# 8 Taarifa ya Meneja kuhusu Uwekezaji

# Taarifa ya Meneja Kuhusu Uwekezaji

UTT AMIS tunatambua umuhimu wa mtoto kwa maendeleo ya Taifa katika siku zijazo. Kwa sababu hiyo, Mfuko wa Watoto (Watoto Fund) ulizinduliwa. Mfuko wa Watoto ni suluhisho la kifedha ambalo linalenga katika kukuza mtaji kwa faida ya muda mrefu kwa ajili ya maendeleo ya watoto wetu wapendwa. Mfuko huu ni wa wazi wenye lengo la kukuza mtaji.


Watoto wote wenye umri chini ya miaka 18 wanaweza kujiunga na mpango huu. Kiasi cha awali kinachohitajika kwa uwekezaji ni shilingi 10,000/=. Uwekezaji wa ziada ni kuanzia shilingi 5,000/= na kuendelea ambao unaweza kufanywa kadiri ya mwekezaji awezavyo.

## 1.0 Ukubwa wa Mfuko na Thamani ya Kipande

Hadi kufikia tarehe 30 Juni 2025, mfuko wa Watoto ulikuwa na ukubwa wa shilingi bilioni 31.5.

Ukubwa wa Mfuko umeongezeka kwa shilingi bilioni 12.5 ikilinganishwa na ongezeko la shilingi bilioni 8.3 mwaka 2024. Thamani ya kipande imeongezeka kutoka shilingi 666.5 hadi kufikia shilingi 771.9.

*Chati Na. I: Ukuaji wa mfuko na thamani ya kipande kwa mfuko wa Watoto hadi tarehe 30 Juni, 2025*





## 2.0 Mgawanyo wa Uwekezaji

Katika kipindi cha mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 mwezi Juni 2025, UTT-AMIS PLC kama meneja wa Mfuko alitumia uzoefu na weledi katika kufikia mgawanyo anuai wa rasilimali kwa matakwa ya sera za mfuko wa Watoto. Mgawanyo anuai wa rasilimali za mfuko mwezi Juni 2025 ulikuwa kama inavyoonekana kwenye chati namba II hapo chini:-

*Chati Na. II: Mgawanyo wa uwekezaji katika mfuko wa Watoto tarehe 30 Juni, 2025*

Chati namba II, inaonesha mgawanyo wa uwekezaji katika mfuko wa Watoto ambapo asilimia 71.54 imewekezwa katika Dhamana za serikali za muda mrefu, ikifuatiwa na asilimia 10.28 kwenye Hisa, asilimia asilimia 18.14 kwenye Amana za benki za muda maalum na asilimia 0.04 kwenye Amana za benki za muda mfupi. Aidha, chati hiyo inaonesha kiwango kikubwa cha asilimia kimewekezwa kwenye Dhamana za serikali za muda mrefu ili kuimarisha kiwango cha faida na mapato ya mfuko.




KUANZISHWA

OKTOBA 2008

30 JUNI 2025

THAMANI YA KIPANDE SHILINGI 771.9

UKUBWA WA MFUKO SHILINGI BILIONI 31.5

FAIDA YA MWAKA 15.8%

## 3.0 Faida

Kiwango cha faida kwa kipindi cha mwaka mmoja ni asilimia 15.8 ikilinganishwa na faida ya asilimia 14.1 mwaka 2024. Aidha, kiwango cha faida kwa mwaka 2025 cha asilimia 15.8 ni zaidi ya kigezo cha ufanisi cha asilimia 12.1 kama inavyonekana kwenye (Jedwali I).

Jedwali namba I na II, linaonesha mwenendo wa utendaji wa Mfuko pamoja na kigezo cha ufanisi (benchmark) kwa mwaka 2021 hadi 2025. Hali ya utendaji wa Mfuko inaonekana ni nzuri na shindani ikilinganishwa na faida ya kigezo cha ufanisi na maeneo linganifu sokoni.

***Jedwali Na. I: Faida ya mfuko wa Watoto tangu Juni, 2021 hadi Juni, 2025***

| Na. | Mwaka wa Fedha | Ukubwa wa mfuko Shilingi Bilioni | Hali ya Utendaji | |
|---|---|---|---|---|
| | | | Faida | Kigezo cha ufanisi |
| 01. | 2024/25 | 31.5 | 15.8% | 12.1% |
| 02. | 2023/24 | 19.0 | 14.1% | 11.2% |
| 03. | 2022/23 | 10.7 | 12.4% | 7.6% |
| 04. | 2021/22 | 5.7 | 14.1% | 8.7% |
| 05. | 2020/21 | 4.2 | 19.9% | 8.1% |

*Kumb:kigezo cha ufanisi ni mjumuiko wa utendaji wa Fahilisi za hisa kwa kampuni za ndani (TSI) na faida kwenye dhamana ya serikali ya miaka 10.*

Ili kupima mafanikio ya mfuko inabidi kulinganisha na viwango vya faida vinavyotolewa na soko kwenye amana za benki na dhamana za serikali kama vinavyoonekana kwenye jedwali namba II hapo chini:

***Jedwali Na. II: Viwango vya faida katika Dhamana za Serikali na Amana za benki***

| Maelezo | Kwa Mwaka Wa Fedha Ulioisha Mwezi Juni | | | |
|---|---|---|---|---|
| | **2022** | **2023** | **2024** | **2025** |
| Dhamana ya Serikali ya Miaka 10 | 10.3% | 11.1% | 12.3% | 14.2% |
| Dhamana ya Serikali ya Miaka 7 | 9.3% | 9.7% | 9.7% | 9.7% |
| Dhamana ya Serikali ya Miaka 5 | 8.9% | 9.7% | 10.0% | 12.9% |
| Dhamana ya Serikali ya Miaka 2 | 4.4% | 9.1% | 11.6% | 12.0% |
| Dhamana ya Serikali ya Mwaka 1 | 4.7% | 6.9% | 8.3% | 8.8% |
| Amana za benki | 1.5% | 1.6% | 2.8% | 2.9% |

*Chanzo; Benki Kuu ya Tanzania*

Mambo mengine muhimu ya kuzingatia wakati wa kulinganisha faida za uwekezaji katika Mfuko wa Watoto na amana katika benki;

- Viwango vya faida vinavyooneshwa hapo juu kwa uwekezaji chini ya miaka mitatu ni kabla ya kutoa kodi ya zuio (withholding tax) ya 10% wakati faida ya mfuko wa Watoto ni baada ya kutoa kodi ya zuio ya 10%.
- Mfuko wa Watoto unaruhusu wanachama wake kuuza vipande vyao wakati wowote hivyo kumpa fursa mwekezaji kupata fedha pindi anapozihitaji na kwamba hakuna kiwango cha chini cha uwekezaji kinachoruhusu kupata faida.
- Viwango vya faida kwenye mfuko vinatolewa sawa kwa wawekezaji wote (wawekezaji wa kipato kidogo, wa kipato cha kati na wale wenye kipato kikubwa).
- Urahisi wa kuongeza na kutoa fedha, aidha mtu anaweza kununua na kuuza viapande muda wowote
- Kuwekeza kwenye mfuko wa Watoto kuna faida zaidi ya kuwa na akaunti ya amana kwa sababu inamuongezea mwekezaji kipato kikubwa kutokana na viwango bora vinavyotolewa na mfuko zaidi ya viwango vya amana vilivyopo kwenye soko la fedha.

## 4.0 Mwenendo wa Uchumi, Tanzania

### 4.1 Pato la Taifa

Kwa mwaka 2024, uchumi wa Tanzania unakadiriwa kukua kwa asilimia 5.5 na unatarajiwa kukua kwa asilimia 6.0 mwaka 2025. Ukuaji huu wa asilimia 5.5 ni mkubwa ukilinganishwa na asilimia 5.1 iliyonakiriwa mwaka 2023. Kwa mujibu wa Ripoti ya Uhimilivu wa Kifedha iliyotolewa na Benki Kuu ya Tanzania, mafanikio haya yamechangiwa na mambo kadhaa, ikiwa ni pamoja na muendelezo wa utekelezwaji wa miradi ya kimkakati ya miundombinu na juhudi za serikali za kuboresha mazingira ya uwekezaji.

*Jedwali Na. III: Mwenendo wa ukuaji wa Pato Halisi la Taifa*

| Mwaka | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 | 2025 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Pato halisi la Taifa | 7.0% | 4.8% | 4.9% | 4.7% | 5.1% | 5.5% | 6.0%* |

Ongezeko chanya la ukuaji wa uchumi linaloonekana tangu mwaka 2022 linaashiria kuwa biashara na shughuli za maendeleo zimefanya vizuri. Aidha, viashiria vinaonyesha kuwa kiwango cha uwekezaji na shughuli sokoni viliongezeka ikilinganishwa na mwaka uliopita. Soko la mitaji na dhamana limeshuhudia kuongezeka kwa wasimamizi wapya wa mifuko ya uwekezaji wa pamoja na kuwepo kwa fursa mpya za Uwekezaji ambazo ziliwavutia wawekezaji kwa kiwango zaidi ya matarajio.

Mwaka 2025, kiasi na thamani ya miamala imeongezeka ikilinganishwa na kipindi kama hicho mwaka uliopita. Kwa upande wa mifuko inayosimamiwa na UTT AMIS, uwepo wa mwenendo mzuri sokoni umeifanya mifuko hiyo kuwa ya kuvutia zaidi sokoni.

### 4.2 Mfumuko wa Bei

Jedwali la IV linaonyesha kuwa kiwango cha mfumuko wa bei kimeendelea kuwa stahimilivu. Kwa mujibu wa Taarifa ya Sera ya Fedha iliyotolewa na Benki Kuu mwezi Julai 2025, kiwango hicho kimeendelea kuwa chini ya kigezo linganifu, cha asilimia 5.0 kilichowekwa na wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC).

Watoto Fund
Faraja kwa Watoto

Nchi ya Tanzania imefanikiwa kudumisha kiwango cha mfumuko wa bei chini ya kigezo linganifu kwa kipindi cha miaka saba mfululizo, kama inavyooneshwa katika Jedwali Na IV. Mamlaka zimekadiria kuwa katika kipindi cha muda wa kati ya miaka mitatu hadi mitano ijayo, mfumuko wa bei utaendelea kubaki chini ya kiwango cha kigezo linganifu.

Hata hivyo, kufikia tarehe 30 Juni 2025, nchi za Rwanda, Jamuhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Sudani Kusini na Burundi zilinakiri kiwango cha mfumuko wa bei cha juu ya kigezo linganifu.

*Jedwali Na. IV: Viwango vya Mfumuko wa Bei*

| Mwaka (Juni) | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 | 2025 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Mfumuko wa Bei | 3.7% | 3.2% | 3.6% | 4.4% | 3.6% | 3.1% | 3. 3% |

Ustahimilivu wa mfumuko wa bei nchini huleta mazingira rafiki kwa wawekezaji na huchagiza maendeleo ya uchumi kwa ujumla. Hali hii husaidia wawekezaji kwenye mifuko inayosimamiwa na UTT AMIS kupata thamani inayokusudiwa bila kuathiriwa kwa kiwango kikubwa na ongezeko la bei za bidhaa na huduma pindi wanapolipwa gawio au kutoa fedha. Vilevile kwa UTT AMIS, hali hii husaidia uwekezaji kuwa thabiti, na hivyo husaidia wawekezaji kutimiza malengo yao ya kifedha ya muda mrefu.

### 4.3 Sekta ya Fedha

Sekta ya fedha nchini Tanzania imeendelea kuchangia kwa kiasi kikubwa katika uchumi. Mwaka 2024, jumla ya mali kwenye mfumo wa fedha nchini ziliongezeka kwa shilingi trilioni 13.3 na kufikia shilingi trilioni 88.6, ambayo ni zaidi ya asilimia 44.2 ya Pato la Taifa (GDP).

Sekta ya fedha inajumuisha sekta ndogo zifuatazo: benki, hifadhi ya jamii, mifuko ya uwekezaji wa pamoja na bima. Sekta ya benki inachukua asilimia 70.2 ya jumla ya mali kwenye mfumo wa fedha, ikifuatiwa na hifadhi ya jamii kwa asilimia 24.1, mifuko ya uwekezaji wa pamoja kwa asilimia 3.0, na sekta ya bima kwa asilimia 2.6.

#### 4.3.1 Sekta ya Benki

Katika mwaka wa fedha ulioishia Juni 2025, utoaji wa huduma za kifedha kupitia njia za kidijitali uliendelea kupata mafanikio makubwa katika soko la ndani. Benki za biashara, kwa kushirikiana na kampuni za mitandao ya simu zinazotoa huduma za pesa mtandao, ziliboresha majukwaa yanayowawezesha watanzania kuweka akiba, kuhamisha fedha, kuwekeza, na kupata mikopo kwa njia ya pesa mtandao.

Unganishwaji wa huduma za simu na benki umesaidia jamii kuongeza imani ya matumizi ya huduma kidijitali. Wawekezaji sasa wanaweza kufanya miamala kutoka/kwenda kwenye akaunti zao za benki na za pesa mtandao kama vile M-Pesa, Mixx by Yas, Halopesa, Azam Pesa, Selcom Pesa na Airtel Money.

Kwa mwaka 2024, kiasi na thamani ya miamala iliofanyika kutoka kwenye akaunti za pesa mtandao kwenda Benki (W2B) kilifikia milioni 9.5 na shilingi trilioni 3.6, ikiwa ni ongezeko la asilimia 43.3 na asilimia 32.7 mtawalia.

Kufikia mwisho wa mwaka wa fedha wa 2024/25, jumla ya rasilimali za sekta ya benki ziliongezeka kwa zaidi ya asilimia 10.0 na kufikia shilingi trilioni 72.4. Ukuaji huu ulitokana na kuongezeka kwa mikopo, ukichagizwa na uwepo wa huduma za benki kidijitali. Jumla ya mikopo na gharama za huduma ziliongezeka kutoka shilingi trilioni 37.4 hadi shilingi trilioni 44.1, huku amana za wateja ziliongezeka kwa asilimia 19.7 kutoka shilingi trilioni 40.6 hadi shilingi trilioni 48.6.

Kampuni ya UTT AMIS imeunganisha mifumo yake na Kampuni za Mitandao ya Simu pamoja na benki. Unganishwaji huu, unasaidia kurahisisha huduma za kuweka akiba na kuwekeza kwenye fursa mabalimbali. Wawekezaji wa mifuko ya UTT AMIS wanaweza kununua vipande wanavyokusudia kwa kuhamisha fedha moja kwa moja kutoka kwenye akaunti zao za pesa mtandao au akaunti za benki bila ya wao kutembelea ofisi husika.

UTT AMIS ilipokea jumla ya shilingi trilioni 1.9 kupitia mifumo iliyounganishwa. Vivyo hivyo, wawekezaji waliuza vipande (kutoa pesa) vyenye thamani ya jumla ya shilingi trilioni 1.3 (repurchases), kiasi kilicholipwa moja kwa moja kwenye akaunti zao za benki.

Watoto Fund
Faraja kwa Watoto

### 4.4 Sekta ya Mawasiliano

Kukua kwa sekta ya mawasiliano nchini kumechangia kwa kiasi kikubwa katika maendeleo ya soko la mitaji na dhamana, hususani katika huduma za kifedha za kidijitali. Huduma za pesa mtandao kama vile M-Pesa, Mixx by Yas, Halopesa, Azam Pesa, Selcom Pesa, na Airtel Money zimetanua zaidi wigo wa huduma za fedha kwa kuwawezesha watumiaji kuweka akiba, kukopa, na kufanya miamala kwa urahisi zaidi.

Idadi ya laini za simu (mkononi na za mezani) ilifikia milioni 92.7 mwezi Juni 2025, ikiwa ni ongezeko la laini milioni 17.2 kutoka mwaka uliopita.  Idadi ya akaunti za pesa mtandao ziliongezeka kwa asilimia 22.0, kutoka milioni 55.7 hadi milioni 68.0. Katika mwaka wa fedha wa 2024/25, idadi ya miamala iliyofanyika kutoka kwenye akaunti za pesa mtandao kwenda UTT AMIS iliongezeka kwa asilimia 26.2, kufikia 276,187, huku thamani ya miamala ikiongezeka kwa asilimia 21.8 hadi shilingi bilioni 86.6.

UTT AMIS kwa kushirikiana na benki za biashara na Kampuni za Mitandao ya Simu (MNOs), imefanikiwa kuunganisha mifumo yake ya malipo na uendeshaji. Wawekezaji sasa wanaweza kufungua akaunti, kujiandikisha, kutoa fedha, na kuona salio kupitia programu tumizi ya UTT AMIS au kwa kupiga msimbo *150*82#. Mwekezaji anaweza kuuza vipande (repurchase) hadi shilingi milioni 5.0 kwa njia ya simu kwa siku.

UTT AMIS inatarajia kuzindua mfumo wa kidijitali kwa wawekezaji kufikia mwisho wa mwaka wa fedha wa 2025/26. Mfumo huu utatoa uwezo kwa wawekezaji kujihudumia wenyewe kwa kufanya shughuli kama usajili, miamala, mawasiliano, na usimamizi wa akaunti, hivyo kurahisisha uwekezaji. Pia, UTT AMIS imeongeza ofisi mpya katika mikoa ya Morogoro, Kahama na Dar es Salaam, na kufanya jumla ya ofisi nchini kufikia nane (8). Ofisi hizi hutumika kama vituo vya elimu ya kifedha, ushirikiano kwa jamii, na msaada kwa wawekezaji.

### 4.6 Viwango vya Riba na Faida

Wastani wa faida kwa dhamana za serikali za muda mfupi iliongezeka hadi asilimia 8.8 mwezi Juni 2025, kutoka asilimia 8.3 mwezi Juni 2024. Vivyo hivyo, Kiwango cha faida kwa mikopo ya siku miongoni mwa benki kiliongezeka hadi asilimia 7.9 kutoka asilimia 7.2.

Viwango vya faida kwa Dhamana za serikali za muda mrefu vilionesha mabadiliko sokoni, hususani katika kipindi cha pili cha mwaka wa fedha 2024/25. Mabadiliko sokoni yalitokea baada ya benki kuu husika kubadili

utaratibu na mfumo wa upatikanaji wa kuponi (faida) za dhamana za serikali. Aidha, utaratibu ulibadilishwa kutoka mfumo wa kuwa na viwango visivyobadilika kwenda mfumo wenye viwango vinavyobadilika kutegemea hali ya soko.

Mabadiliko hayo yalisababisha kupungua kwa viwango vya faida kwa dhamana za muda mrefu na kuongezeka kwa faida kwa dhamana za muda mfupi na wa kati (Jedwali Na. V). Kwa mujibu wa Benki Kuu, mabadiliko haya yalifanyika ili kuakisi hali halisi ya soko kwa wakati huo.

***Jedwali Na. V: Mabadiliko ya Viwango vya Faida (Coupon Rates): Dhamana za Serikali za muda mrefu.***

| Na. | Maelezo | | Miaka 2 | Miaka 5 | Miaka 10 | Miaka 15 | Miaka 20 | Miaka 25 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1.0 | Kabla ya Mabadiliko | Kuponi | 7.60% | 9.18% | 11.44% | 13.50% | 15.49% | 15.95% |
| | | Faida | 11.64% | 12.40% | 13.25% | 15.76% | 15.70% | 15.93% |
| 2.0 | Baada ya Mabadiliko | Kuponi | 12.50% | 13.00% | 14.00% | 14.50% | 15.25% | 15.75% |
| | | Faida | 12.08% | 12.94% | 14.25% | 14.62% | 14.50% | 14.83% |

Viwango vya riba na faida katika benki za biashara, riba za mikopo na faida za amana hazikubadilika kwa kiwango kikubwa ikilinganishwa na mwaka uliopita. Kiwango cha jumla cha riba ya mikopo kilikuwa wastani wa asilimia 15.6, huku kiwango cha mikopo ya mwaka mmoja kikiwa asilimia 15.8. Viwango vya faida kwa amana za jumla na za muda wa mwaka mmoja vilikuwa asilimia 9.7 na asilimia 8.7, mtawalia. Mnamo Januari 2025, Benki Kuu ilibadilisha mfumo wake wa sera ya fedha kutoka kulenga jumla ya fedha kwenye mzunguko hadi kulenga viwango vya faida sokoni. Kufikia Juni 2025, kiwango cha riba cha Benki Kuu (CBR) kwa benki za biashara kilibaki kuwa asilimia 6.0.

Uwepo wa hali stahimilivu ya viwango vya faida na maendeleo ya soko kwa ujumla ni muhimu na husaidia kutoa matarajio chanya kwa wawekezaji na mifuko ya UTT AMIS.

## 4.7 Soko la Kubadilisha Fedha za Kigeni

Hadi tarehe 30 Juni 2025, akiba ya fedha za kigeni nchini ilikuwa zaidi ya Dola za Marekani bilioni 6.0, ambapo Benki Kuu ilikadiria kuwa kiwango hiki kinatosha kwa matumizi ya kulipia huduma na bidhaa kutoka nje ya nchi kwa takribani miezi minne. Dola moja ya Marekani ilibadilishwa kwa shilingi 2,631.3, ikilinganishwa na shilingi 2,640.0 mwezi Juni 2024. Kwa kipindi cha mwaka mmoja, thamani ya shilingi iliongezeka kwa asilimia 0.3, ikilinganishwa na hali ilivyokuwa mwaka jana ambapo thamani ilipungua kwa asilimia 12.8 (Jedwali VI).

Kuendelea kufanya vizuri kwa fedha ya Tanzania kumechagizwa na hatua mbalimbali ambazo mamlaka husika zimechukua ili kuendelea kuimarisha thamani ya fedha yetu. Aidha, hatua zilizochukuliwa ni pamoja na kuzuia matumizi ya fedha za kigeni kwa manunuzi na malipo ya huduma na bidhaa nchini. Vilevile, mwezi Oktoba 2024, Benki Kuu ilianzisha mpango wa kununua dhahabu kama sehemu ya mkakati wake wa kuongeza kiwango cha akiba ya fedha za kigeni. Pamoja na mambo mengine, hatua hizi zinatarajiwa kupunguza mahitaji ya fedha za kigeni na kuimarisha thamani ya shilingi ya Tanzania.

***Jedwali Na. VI: Viwango vya Kubadilisha Fedha za Kigeni Shilingi/USD***

| Mwaka | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 | 2025 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Viwango vya Kubadilisha Fedha | 2,300.9 | 2,307.9 | 2,310.4 | 2,315.7 | 2,339.1 | 2,640.0 | 2,631.3 |

Kuimarika kwa thamani ya fedha ya Tanzania dhidi ya fedha za kigeni ni muhimu kwa mifuko ya UTT AMIS na Uchumi kwa ujumla. Hali hii husaidia faida zitokanazo na uwekezaji kuendelea kuwa nzuri na za kuvutia kwa wawekezaji walio ndani na nje ya nchi. Mifuko ya UTT AMIS hutoa faida shidani ingawa huathiriwa na kuleta mabadiliko ya kiwango cha fedha endapo thamani ya shilingi ya Tanzania inapoongezeka au kupungua.

## 4.8 Soko la Mitaji na Dhamana

Kiwango cha uwekezaji na ushiriki wa wawekezaji katika soko la mitaji na dhamana kiliongezeka katika mwaka wa fedha ulioishia Juni 2025 ikilinganishwa na kipindi kilichopita. Kwa mujibu wa Benki Kuu ya Tanzania na Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA), idadi ya wawekezaji iliongezeka kwa asilimia 16.8

mwaka 2024, na kufikia 1,060,509. Ongezeko hili limechagizwa na maendeleo ya soko, elimu na matumizi ya teknolojia katika uwekezaji, hali ambayo imerahisisha na kuwavutia wawekezaji wa ndani na nje ya nchi.

Miongoni mwa maendeleo ya soko yaliyotekelezwa katika kipindi hicho ni pamoja na mabadiliko ya mfumo wa upatikanaji wa viwango vya faida (coupon rates) na bei za hisa sokoni. Aidha, mabadiliko hayo yameleta mwenendo na hali mpya kwenye viwango vya faida na bei za hisa sokoni.

Katika kipindi cha mwaka mmoja, washirika wengi sokoni wameendelea kutoa kipaumbele zaidi kwenye uwekezaji unaozingatia mazingira, jamii na utawala (ESG) pamoja na maadili ya dini ya kiislamu (Shariah).

#### 4.8.1 Soko la Awali

Katika soko la Dhamana za serikali za muda mfupi, kiasi kilichotolewa kilipungua kwa shilingi trilioni 0.1 na kufikia shilingi trilioni 2.6. Vilevile, upande wa mahitaji, kiasi kilichonakiriwa kilipungua kwa shilingi trilioni 1.0 hadi shilingi trilioni 3.3 kutoka shilingi trilioni 4.3. Jumla ya kiasi kilichochukuliwa kilipungua kwa shilingi trilioni 0.7 kutoka shilingi trilioni 2.6 hadi shilingi trilioni 1.9 mwaka 2025.

Kwenye soko la Dhamana za serikali za muda mrefu, Kiwango cha mauzo na ushiriki sokoni kiliongezeka ikilinganishwa na kipindi kilichopita. Aidha, kwa kipindi hicho kiwango kikubwa cha uwekezaji kilifanyika kwenye dhamana za muda mrefu ikilinganishwa na zile za muda mfupi sokoni.

Jumla ya shilingi trilioni 4.2 zilitolewa kwa mauzo ikilinganishwa na shilingi trilioni 3.3 mwaka uliopita. Kiasi kilichopokelewa na Benki Kuu kiliongezeka kwa shilingi trilioni 2.0 hadi shilingi trilioni 7.2 ikilinganishwa na shilingi trilioni 5.2 mwaka jana. Kiasi kilichofanikiwa kuchukuliwa kiliongezeka kwa shilingi trilioni 1.0 hadi shilingi trilioni 3.8 kutoka shilingi trilioni 2.8 mwaka 2024.

Katika soko la Hatifungani za kampuni binafsi, soko limenakiri ongezeko la shughuli nyingi kwa upande wa mauzo, washiriki wapya, na mengineyo. Katika kipindi hicho, benki tano za biashara zilitangaza fursa za uwekezaji wenye thamani ya shilingi trilioni 1.2, kama inavyoonyeshwa katika Jedwali VII.

*Jedwali VII: Orodha ya Hatifungani za Kampuni binafsi zilizoorodheshwa*

| Idadi | Taasisi / Kampuni | Maelezo | Muda | Faida | Tarehe iliyotolewa | Zaidi (-)/chini (+) ya matarajio |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1.0 | Benki ya PBZ | SUKUK Bond | Miaka 7 | 10.5% | 17 Feb 2025 | -12.0% |
| 2.0 | Benki ya CRDB | Samia Infrastructure Bond | Miaka 5 | 12.0% | 10 Feb 2025 | -215.4% |
| 3.0 | Benki ya Azania | Bondi Yangu | Miaka 3 | 12.5% | 17 Jan 2025 | -210.9% |
| 4.0 | Benki ya NBC | Twiga Bond | Miaka 5 | 10.75 | 10 Oct 2024 | -130.0% |
| 5.0 | Benki ya Stanbic | Stanbic Bond | Miaka 5 | 12.5% | 11 Oct 2024 | Haihusiani |

Katika kipindi hadi Juni 2025, soko la Mifuko ya uwekezaji wa pamoja nchini liliendelea kukua na kufanya vizuri ikilinganishwa na kipindi kilichopita. Kwa kipidi hicho, soko lilionesha ongezeko la wasimamizi, mifuko mipya na idadi ya wawekezaji. Hata hivyo, mifuko mipya iliyoanzishwa, inaashiria ukuaji wa soko na kuimarika kwa utamaduni wa kujiwekea akiba miongoni mwa watanzania na wawekezaji wote kwa ujumla.

#### 4.8.2 Soko la Upili

Katika soko la Upili, jumla ya miamala ya Dhamana za serikali iliyofanyika ilikua kwa shilingi trilioni 0.7 na kufikia shilingi trilioni 4.2 ikitoka shilingi trilioni 3.5 mwaka uliopita.

Kwa Hatifungani za kampuni binafsi zilizoorodheshwa, thamani ya miamala ilikuwa shilingi bilioni 9.3 ikilinganishwa na shilingi bilioni 3.9 mwaka jana. Aidha, ongezeko la thamani ya miamala ya hatifungani kwa kipindi hicho lilisababishwa na uwepo wa hatifungani mpya na mauzo ya hatifungani zilizokuepo sokoni.

#### 4.8.3 Soko la Hisa

Kufikia tarehe 30 Juni 2025, ukubwa wa soko la Hisa la Dar es Salaam (DSE) ulifikia shilingi trilioni 19.6, ikiwa ni ongezeko la shilingi trilioni 2.8 kutoka shilingi trilioni 16.8 iliyonakiriwa tarehe 30 Juni 2024. Wastani wa ushiriki sokoni kwa wawekezaji wa ndani ya nchi ni asilimia 90.6, ikilinganishwa na asilimia 76.2 mwaka 2024.

Fahirisi ya Hisa za kampuni za ndani (TSI), ambayo hufuatilia utendaji wa kampuni zilizoorodheshwa nchini, iliongezeka kwa asilimia 8.4 hadi kufikia 4,852.3. Fahirisi ya kampuni zote sokoni (DSEI) ikijumuisha zile za nje na ndani ya nchi iliongezeka kwa asilimia 16.7 na kufunga mwaka katika kiwango cha 2,353.8. Jumla ya

mauzo ya soko katika kipindi hicho yaliongezeka kwa shilingi bilioni 134.9 hadi shilingi bilioni 407.3 kutoka shilingi bilioni 272.4 mwaka uliopita.

Baadhi ya kampuni zilizoorodheshwa zilitangaza na kulipa gawio kwa wanahisa kama ifuatavyo:TCC: shilingi 850 kwa kila hisa, TPCC: shilingi 600 kwa kila hisa, TBL: shilingi 1,259 kwa kila hisa, NMB: shilingi 428.85 kwa kila hisa, SWISS: shilingi 70.72 kwa kila hisa, VODA: shilingi 20.2 kwa kila hisa, DSE: shilingi 125.5 kwa kila hisa na CRDB: shilingi 65 kwa kila hisa.

#### 4.8.4 Mifuko ya Uwekezaji wa Pamoja (CIS)

Uwekezaji katika Mifuko ya Uwekezaji wa Pamoja (CIS) uliendelea kufanya vizuri katika mwaka wa fedha ulioishia mwezi Juni 2025. Katika kipindi hicho, idadi ya wasimamizi na mifuko iliongezeka sokoni ikilinganishwa na kipindi kilichopita.

Hadi tarehe 30 mwezi Juni 2025 ukubwa wa mifuko sokoni ulifikia shilingi bilioni 3,272.3 ukilinganishwa na shilingi bilioni 2,273.6 ulionakiriwa mwaka 2024.

##### 4.8.4.1 Mifuko na Huduma za UTT AMIS

Katika mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni 2025, jumla ya thamani ya rasilimali ya mifuko inayosimamiwa (AUM) na UTT AMIS iliongezeka kwa shilingi bilioni 1,030.5, ikilinganishwa na ongezeko la shilingi bilioni 702.8 lililonakiriwa mwaka 2024. Aidha, jumla ya rasilimali ziliongezeka kutoka shilingi bilioni 2,238.2 hadi shilingi bilioni 3,268.7. Ongezeko hilo la rasilimali, linaashiria kuongezeka kwa imani ya wawekezaji katika fursa za uwekezaji zinazosimamiwa na UTT AMIS.

Kwa upande wa UTT AMIS, kuingia kwa wasimamizi wapya wa mifuko ya uwekezaji na fursa zingine mpya ni kiashiria chanya cha ukuaji na kuimarika kwa imani katika soko la mitaji na dhamana. Uwepo wa fursa mpya za uwekezaji, na kuongezeka kwa wasimamizi wa mifuko nchini kunasaidia kukuza utamaduni wa kujiwekea akiba, huongeza ukwasi, na kuchochea ushindani wenye afya sokoni.

Kutokana na hayo, hali ya utendaji wa mifuko ya UTT AMIS kwa ujumla ilikuwa imara ikilinganishwa na maeneo mengine linganifu. Faida iliyopatikana na ukwasi uliotolewa kwa wawekezaji kwa mwaka wa fedha wa 2024/25 ilikuwa ya kuvutia na shindani. Hivyo basi, tunajivunia mafanikio yetu kwa pamoja na kuahidi kuendelea kutoa huduma bora itakayo kidhi matarajio ya wawekezaji tulionao sasa na hata wale watakaowekeza nasi kwa siku zijazo.

### 4.9 Huduma Jumuishi Za Kifedha

Kukua kwa huduma jumuishi za kifedha nchini Tanzania zimechochewa kwa kiasi kikubwa na maendeleo ya kiteknolojia na ubunifu wa huduma na bidhaa. Kwa mujibu wa taarifa ya mwaka ya Ujumuishaji wa matumizi ya huduma na bidhaa za kifedha iliyotolewa na Benki kuu, idadi ya vituo vya upatikanaji wa huduma za kifedha iliongezeka kwa asilimia 9.7 mwaka 2024, kufikia vituo 417, ikiwa ni ongezeko kubwa ikilinganishwa na asilimia 2.3 ya mwaka 2023. Ukuaji huu ulitokana hasa na kuongezeka kwa idadi ya vituo, Mifuko ya Uwekezaji wa Pamoja (CIS), Wasimamizi wa Mifuko, madalali wa soko la Hisa la Dar Es Salaam (LDM), Washauri wa Uwekezaji, na waangalizi wa mifuko.

Kwa upande wa UTT AMIS, hadi tarehe 30 Juni 2025, jumla ya rasilimari zinazosimamiwa na Taasisi ya UTT AMIS ni shilingi trilioni 3.2. Kiasi hiki cha fedha kinatafsiri jumla ya thamani ya uwekezaji uliowekezwa kwenye soko la dhamana na mitaji nchini kwa niaba ya wawekezaji kwa kipindi hicho. Aidha, uwekezaji kwenye mifuko ya UTT AMIS huwekezwa kwenye maeneo kama vile, hatifungani za kampuni binafsi na hisa zilizoorodheshwa, amana za benki, na dhamana za serikali. Mifuko hii huwapa Watanzania fursa ya kuwekeza zaidi ya akaunti za kawaida za akiba.

Taasisi ya UTT AMIS kupitia mifuko yake, tumeweza kuanzisha kampeni mbalimbali, ili kuhamasisha umma kuwa na utamaduni wa kujiwekea akiba. Taasisi, imeanzisha programu na kampeni mbalimbali kama vile Kijiwe Mchongo na imehamasisha umma kuwekeza kwa kidijitali. Elimu inayotolewa na mafanikio yaliyopatikana kwa kipindi cha miaka 20 iliyopita yamewezesha jamii kufikia malengo yake na kudumisha zaidi utamaduni wa kuweka akiba na kuwekeza kwenye soko la dhamana na mitaji nchini.

Kwa kipindi cha mwaka mmoja, UTT AMIS ilifanikisha kufungua akaunti mpya 134,768 kupitia simu za mkononi za wawekezaji, na kufanya uwekezaji (kununua vipande) wenye thamani ya shilingi bilioni 86.6. Hata hivyo, wawekezaji waliuza vipande kwa njia ya simu za mkononi vyenye thamani ya shilingi bilioni 235.2, kiasi ambacho kililipwa kwenye akaunti zao za benki.

Kupitia mchakato wake wa usajili wa wawekezaji, UTT AMIS imehamasisha Watanzania wengi kufungua akaunti za benki, ambazo huhitajika wakati wa kujiunga na ni lazima wakati wa kutoa fedha (kuuza vipande). Zaidi ya hayo, UTT AMIS imewezesha upatikanaji wa mikopo kutoka Taasisi za kifedha kwa kuwaelimisha wawekezaji kuhusu elimu ya fedha na kuruhusu kutumia fedha walizowekeza kama dhamana dhidi ya mkopo.

***Chanzo:*** *Benki kuu ya Tanzania, Ofisi ya Taifa ya Takwimu, UTT AMIS na Soko la Hisa la Dar es Salaam.*

***Bodi na Wafanyakazi wa UTT AMIS tunawatakia wote***
***Msimu wa Sikukuu wenye Furaha na Mafanikio katika mwaka wa 2026.***

***Wekeza Uwezeshwe!***

Watoto Fund
Faraja kwa Watoto

# 9 Jarida la Habari

# Jarida la habari la UTT AMIS
# [Hadi tarehe 30 Septemba, 2025]

## 1.0 Maelezo Mafupi juu ya Kampuni ya Uwekezaji ya UTT AMIS

- Hadi kufikia tarehe 30 Septemba 2025, Kampuni ya uwekezaji ya UTT AMIS inasimamia jumla ya mifuko ya uwekezaji wa pamoja sita (6) ambayo ni : Mfuko wa Umoja, Mfuko wa Wekeza Maisha,Mfuko wa Watoto, Mfuko wa Jikimu, Mfuko wa Ukwasi na Mfuko wa Hatifungani.
- UTT AMIS inasimamia rasilimali zenye jumla ya thamani ya zaidi ya shilingi Trilioni 3.6
- Mwaka 2017 Kampuni ya UTT AMIS ilianzisha huduma ya usimamizi mali kwa kampuni na watu binafsi iitwayo UTT WEALTH MANAGEMENT yenye uwekezaji wenye thamani zaidi ya shilingi bilioni 43.1.
- Wawekezaji ni zaidi ya **558,768.**
- Mifuko hii ya uwekezaji wa pamoja hutoa faida shindani na ukwasi ukilinganisha na maeneo mengine linganifu sokoni.

## 2.0 Taarifa za ujumla za Mifuko na huduma iliyoanzishwa na kusimamiwa na kampuni ya UTT AMIS

| NA | JINA LA MFUKO | MAELEZO |
|---|---|---|
| 2.1 | Mfuko wa Umoja | Mfuko ulianzishwa tarehe 16 Mei, 2005. Mfuko huu unalenga zaidi wawekezaji wenye malengo ya muda wa kati na mrefu, jambo ambalo huwawezesha kupata muda wa kutosha kujiwekea akiba na kukuza mtaji wao. Mfuko unawekeza katika soko la mitaji na dhamana zilizoorodheshwa. |

**Sifa za mfuko ni:**

- Vipande vinauzwa kwa thamani halisi [hakuna gharama za kujiunga].
- Wawekezaji ni watu binafsi, vikundi na Taasisi, unaruhusiwa katika mfuko huu.
- Kiwango cha chini cha kujiunga ni vipande 10.
- Gharama ya kujiondoa inayotozwa ni 1% ya thamani halisi ya kipande.
- Mauzo ya vipande hufanyika ndani ya siku 10 za kazi baada ya maombi kupokelewa katika ofisi za UTT AMIS.
- Mwekezaji akifariki mrithi, mwakilishi au mwombaji wa pili ataruhusiwa kuendeleza uwekezaji huo.
- Vipande vinaweza kutumika kama dhamana ya mkopo katika Taasisi za fedha.

*Jedwali Na. 01; Faida kwa kipindi hadi tarehe 30 Septemba 2025*

| Tangu Kuanzishwa [Mei,2005] | Miaka 15 | Miaka 10 | Miaka 5 | Miaka 2 | Mwaka 1 |
|---|---|---|---|---|---|
| 15.1% | 16.8% | 15.5% | 16.6% | 12.0% | 11.4% |

*Chati Na. 01; Ukubwa wa Mfuko na Thamani ya Kipande tangu kuanzishwa hadi 30 Septemba 2025*



**2.2 Mfuko wa Wekeza Maisha**

Mfuko ulianzishwa tarehe 16 Mei, 2007. Mfuko huu unatoa faida za aina 2 ambazo ni, faida ya kukuza mtaji pamoja na faida ya bima. Katika Mfuko huu, zaidi ya asilimia 99.0 ya rasilimali huwekezwa na kiasi kilichobaki hupelekwa katika huduma za bima. Mfuko unawekeza katika soko la mitaji na dhamana.

**Sifa za mfuko;**


- Mfuko unaruhusu mwekezaji mwenye umri kati ya miaka 18 hadi 55 kujiunga.
- Mfuko una aina mbili za mpango wa kuwekeza: (a) kuwekeza kwa awamu na (b) kuwekeza kwa mkupuo.
- Vipande vinauzwa kwa thamani halisi ya wakati huo [hakuna gharama za kujiunga].
- Kwa mpango wa kuwekeza kila mwezi, kiwango cha chini ni shilingi 8,340/= (ikiwa mwekezaji ana lengo la kufikia kiasi cha shilingi Milioni Moja kwa miaka 10).
- Faida za bima zinazopatikana ni: - bima ya maisha, bima ya ajali, bima ya ulemavu wa kudumu na gharama za mazishi.
- Mfuko unampa fursa mwekezaji kuwekeza kwa mpangilio maalumu, mathalani anaweza kuchagua kuchangia kwa mwezi, mara mbili kwa mwaka au mara moja kwa mwaka.
- Mfuko unampa fursa mwekezaji kupanga na kuchagua lengo na mpango wa uwekezaji atakaoutekeleza na kuutimiza ndani ya miaka 10.
- Mwekezaji akifariki mrithi au mwakilishi au mwombaji wa pili ataruhusiwa kuendeleza uwekezaji.

Watoto Fund
Faraja kwa Watoto

***Jedwali Na. 02; Faida kwa kipindi hadi tarehe 30 Septemba 2025***

| Tangu Kuanzishwa [Mei,2007] | Miaka 10 | Miaka 5 | Miaka 2 | Mwaka 1 |
|---|---|---|---|---|
| 13.9% | 25.5% | 22.3% | 14.6% | 14.3% |

***Chati Na. 02; Ukubwa wa Mfuko na Thamani ya Kipande tangu kuanzishwa hadi 30 Septemba 2025***



Watoto Fund
Faraja kwa Watoto

2.3 **Mfuko wa Watoto**

Mfuko ulianzishwa tarehe 01 Oktoba 2008. Mfuko una lengo la kuwanufaisha watoto kwa kujiwekea akiba na kutumia uwekezaji wao kukidhi gharama za shule na kupata mtaji kwa maendeleo ya baadae. Mfuko unawekeza katika soko la mitaji na dhamana.


**Sifa za Mfuko;**

- Uwekezaji ni kwa ajili ya mtoto mwenye umri chini ya miaka 18.
- Kiwango cha chini cha uwekezaji ni shilingi 10,000/= na kiwango cha nyongeza ni kuanzia shilingi 5,000/= na kuendelea.
- Vipande vinauzwa kwa thamani halisi ya wakati huo. [ hakuna gharama za kujiunga ]
- Mfuko unatoa Mpango wa kukuza mtaji.
- Mzazi au Mlezi ataruhusiwa kuuza au kupunguza sehemu ya uwekezaji wake pindi mtoto atakapofikisha umri wa miaka 12.
- Taasisi, kampuni na vikundi vinaweza kuwawekezea watoto kama sehemu ya huduma kwa jamii

*Jedwali Na. 03; Faida kwa kipindi hadi tarehe 30 Septemba 2025*

| Tangu Kuanzishwa [Okt,2008] | Miaka 10 | Miaka 5 | Miaka 2 | Mwaka 1 |
|---|---|---|---|---|
| 13.1% | 18.1% | 20.7% | 15.9% | 15.1% |

*Chati Na. 03; Ukubwa wa Mfuko na Thamani ya Kipande tangu kuanzishwa hadi 30 Septemba 2025*



| | | |
|---|---|---|
| 2.4 | **Mfuko wa Jikimu** | Mfuko ulianzishwa tarehe 03 Novemba 2008. Lengo la mfuko ni kuwawezesha wawekezaji kupata gawio kutokana na mapato ya ziada katika vipindi tofauti na kukuza mtaji kwa mwekezaji wa muda mrefu. Mfuko unawekeza katika soko la mitaji na dhamana. |

Jikimu Income Scheme

LIVE WELL ...YOU DESERVE IT

**Sifa za Mfuko:**

Aina ya mpango wa uwekezaji

- (a) Mpango wa kukuza mtaji ni kuanzia shilingi. 5,000/= (b) Mpango wa kupata gawio kila robo mwaka (Kiwango cha chini cha uwekezaji ni shilingi milioni 2) na (c) Mpango wa kupata gawio kwa mwaka (kiwango cha chini cha uwekezaji ni shilingi milioni 1).
- Kiwango cha nyongeza ni kuanzia shilingi 5,000/= kwa mpango wa kukuza mtaji na shilingi 15,000/= kwa mpango wa kupata gawio.
- Vipande vinauzwa kwa thamani halisi ya wakati huo [ hakuna gharama za kujiunga]
- Mfuko unatoza gharama za kujitoa kama ifuatavyo: (a) 2.0% kwa mwekezaji aliedumu ndani ya mfuko kwa kipindi kisichozidi mwaka mmoja. (b) 1.5% kwa mwekezaji aliedumu ndani ya mfuko kwa kipindi cha zaidi ya mwaka 1 na chini ya miaka 2. (c) 1% kwa uwekezaji uliodumu ndani ya mfuko kwa kipindi cha zaidi ya miaka 2 na chini ya miaka 3 na, (d) Uwekezaji uliodumu ndani ya mfuko kwa kipindi cha zaidi ya miaka 3 hakuna gharama za kujitoa.
- Ni rahisi kwa mwekezaji kupata fedha pindi anapohitaji (ndani ya siku 10 za kazi baada ya maombi ya kuuza vipande kupokelewa katika ofisi za UTT AMIS).
- Vipande vinaweza kutumika kama dhamana ya mkopo katika Taasisi za fedha.
- Mwekezaji akifariki mrithi, mwakilishi au mwombaji wa pili ataruhusiwa kuendeleza uwekezaji.


***Jedwali Na. 04; Faida kwa kipindi hadi tarehe 30 Septemba 2025***

| Tangu Kuanzishwa [Nov, 2008] | Miaka 10 | Miaka 5 | Miaka 2 | Mwaka 1 |
|---|---|---|---|---|
| **17.5%** | 15.2% | 18.4% | 15.7% | 14.0% |

***Jedwali Na. 05; Gawio kwa kipindi hadi tarehe 30 Septemba 2025***

| Taarifa | Shilingi Bilioni | Kwa kila kipande, shilingi |
|---|---|---|
| Tangu Kuanzishwa [Nov, 2008] | 18.0 | 197.5 |
| Mwaka Mmoja [Okt 24-Sept 25] | 1.1 | 12.0 |

***Chati Na. 04; Ukubwa wa Mfuko na Thamani ya Kipande tangu kuanzishwa hadi 30 Septemba 2025***



## 2.5 Mfuko Wa Ukwasi (Liquid Fund)

Mfuko ulianzishwa tarehe 01 Machi, 2013. Ni Mfuko wa wazi ambao unatoa fursa kwa wawekezaji wenye lengo la muda mfupi, wa kati na mrefu. Ni mfuko wa wazi ambao rasilimali zake huwekezwa katika maeneo yenye vipato vya kudumu (fixed income instruments).

**Sifa za mfuko:**


- Kiwango cha chini cha uwekezaji ni shilingi 100,000/= na kiwango cha nyongeza kisichopungua shilingi 10,000/=.
- Ni rahisi kwa mwekezaji kupata fedha zake za mauzo ya vipande, (ndani ya siku 3 za kazi baada ya maombi ya kuuza vipande kupokelewa katika ofisi za UTT AMIS)
- Mfuko hauna gharama yoyote ya kujiunga wala kujitoa.
- Mfuko unaruhusu watu binafsi,vikundi au Taasisi kuwekeza.
- Vipande vinauzwa kwa thamani halisi ya wakati huo (hakuna gharama za kujiunga).
- Vipande vinaweza kutumika kama dhamana ya mkopo katika Taasisi za fedha.
- Mwekezaji akifariki mrithi, mwakilishi au mwombaji wa pili anaruhusiwa kuendeleza uwekezaji.

Watoto Fund
Faraja kwa Watoto

*Jedwali Na. 06; Faida kwa kipindi hadi tarehe 30 Septemba 2025*

| Tangu Kuanzishwa [Machi, 2013] | Miaka 10 | Miaka 5 | Miaka 2 | Mwaka 1 |
|---|---|---|---|---|
| 18.5% | 16.0% | 17.3% | 14.0% | 13.2% |

*Chati Na. 05; Ukubwa wa Mfuko na Thamani ya Kipande tangu kuanzishwa hadi 30 Septemba 2025*



## 2.6 Mfuko wa Hatifungani (Bond Fund)

Mfuko ulianzishwa tarehe 16 Septemba, 2019. Ni mfuko wa wazi ambao rasilimali zake huwekezwa katika maeneo yenye vipato vya kudumu (fixed income instruments). Mfuko una lengo la kutoa gawio, kulingana na faida itakayopatikana na kukuza mtaji kwa wawekezaji wa muda mrefu.

**Sifa za mfuko:**

Kuna aina tatu za mpango wa uwekezaji katika Mfuko huu:

- Mpango wa kukuza mtaji
- Mpango wa gawio kila mwezi na
- Mpango wa gawio kila baada ya miezi sita.

Kiwango cha chini cha kuanza kuwekeza.

(a) Shilingi 50,000 kwa mpango wa kukuza mtaji

(b) Shilingi milioni 10 kwa mpango wa gawio kila mwezi na

(c) Shilingi milioni 5 kwa mpango wa gawio kila baada ya miezi sita.

- Ni rahisi kwa mwekezaji kupata fedha pindi anapohitaji, (ndani ya siku 10 za kazi baada ya kupokelewa katika ofisi za UTT AMIS).
- Vipande vinaweza kutumika kama dhamana ya mkopo katika taasisi za fedha.
- Mwekezaji akifariki mrithi, mwakilishi au mwombaji wa pili anaruhusiwa kuendeleza uwekezaji.


***Jedwali Na. 07; Faida kwa kipindi hadi tarehe 30 Septemba 2025***

| Tangu Kuanzishwa [Sept,2019] | Miaka 5 | Miaka 2 | Mwaka 1 |
|---|---|---|---|
| 16.1% | 14.7% | 13.2% | 13.4% |

***Jedwali Na. 08; Gawio kwa kipindi hadi tarehe 30 Septemba 2025***

| Taarifa | Shilingi Bilioni | Kwa kila kipande, shilingi |
|---|---|---|
| Tangu Kuanzishwa [Sept,2019] | 107.4 | 69.0 |
| Mwaka Mmoja [Okt 24 - Sept 25] | 38.1 | 12.0 |

***Chati Na. 06; Ukubwa wa Mfuko na Thamani ya Kipande tangu kuanzishwa hadi 30 Septemba 2025***



2.7 **Huduma ya usimamizi mali / UTT Wealth Management**

Huduma hii ilianzishwa mnamo mwaka 2017, kwa kuweka kipaumbele malengo ya kifedha ya watu binafsi, familia, vikundi na Taasisi za ndani na nje ya nchi. Huduma hii hutengeneza uwekezaji kulingana na mahitaji na malengo ya mwekezaji.

**Sifa za huduma hii:**

- Kiwango cha chini cha kuwekeza ni shilingi milioni 100 na kiwango cha nyongeza ni kuanzia shilingi Milioni 10. Uwekezaji unaweza kutumika kama dhamana.
- Huduma hii inampa fursa mwekezaji kuwekeza kwenye uwekezaji wa muda mrefu sokoni huku akipata nafasi ya kuongeza au kuuza sehemu ya uwekezaji wake kulingana na hali ya soko.
- Katika kufanikisha huduma hii mwekezaji atalipia asilimia 1.0 kwa mwaka kama gharama ya usimamizi wa rasilimali zake.
- Uwekezaji katika huduma hii, unatoa fursa kwa wawekezaji kuchagua mpango wa kupata malipo ya faida kila baada ya miezi 6 na mpango wa kukuza mtaji.
- Mwekezaji akifariki mrithi, mwakilishi au mwombaji wa pili ataruhusiwa kuendeleza uwekezaji

***Chati Na. 05; Mwenendo wa Rasilimali kwa Huduma ya Usimamizi Mali, tangu kuanzishwa hadi 30 Septemba 2025***




## 3.0 Elimu kwa Wawekezaji

3.1 **Unawezaje kujiunga na Mifuko ya UTT AMIS?**

Mtanzania mkazi na asiye mkazi, mtu binafsi, Taasisi, vikundi wawekezaji wawili (Jointly) wanaruhusiwa ku wekeza katika Mifuko inayosimamiwa na UTT AMIS. Jinsi ya kuwekeza :

- Mwekezaji binafsi anaweza kujiunga kwa kubonyeza *150*82# na kujisajili kwenye programu tumizi (UTT AMIS APP) ambayo inaweza kupakuliwa kwenye 'App Store' au 'PlayStore'
- Mwekezaji anatakiwa kujaza fomu ya kufungua akaunti kwa ajili ya kukamilisha usajili (KYC FORM).
- Kikundi na Taasisi, wawekezaji wawili (Joint) atajaza fomu ya kufungua akaunti ya UTT AMIS pamoja na viambatanisho vinavyotambulika kisheria (Certificate of Registration,Muhtsari wa Kikao, NIDA za Watia saini n.k) na kuvituma kupitia barua-pepe uwekezaji@uttamis.co.tz au kuleta kwenye Ofisi za UTT AMIS zilizo karibu nawe au Tawi lolote la CRDB au Madalali wote walioidhinishwa na Soko la Hisa la Dar es salaam. Kwa wawekezaji walio nje ya nchi, kwa akaunti ya mtu binafsi au watu wawili watajaza fomu ya kufungua akaunti na kisha kuambatanisha kitambulisho cha uraia.
- Baada ya kupata akaunti namba ya Mfuko uliouchagua na kukamilisha taratibu zote za usajili (KYC Form) mwekezaji anaweza kuanza na kuendelea kuwekeza kupitia njia za simu kama vile Mixx by Yas, Mpesa, AirtelMoney, Halopesa. T-Pesa, Azam Pesa na Ezypesa au njia za kibenki kupitia CRDB, NMB, NBC, STANBIC na zingine.

**3.2 Nini maana ya kiwango cha Mfumuko wa bei? Na jinsi gani inamuathiri mwekezaji?**

Kwa tafsiri rahisi, mfumuko wa bei ni alama inayotafsiri mabadiliko ya bei za bidhaa na huduma kwa kipindi fulani sokoni. Kuongezeka kwa kiwango cha mfumuko wa bei huashiria kupungua kwa thamani ya fedha au kuongezeka kwa bei za bidhaa na huduma sokoni.

Kuna sababu nyingi za kiuchumi zinazopelekea kutokea kwa hali hii, hususani ongezeko la fedha katika mzunguko kusikoendana na kasi ya ukuaji wa uchumi na hivyo matokeo yake kupelekea mfumuko wa bei.

Kiujumla, vigezo vilivyokubalika kupima viwango vya mfumuko wa bei ni pamoja na Bei za bidhaa za Jumla (Wholesale Price Index)], Bei za mahitaji ya kawaida ya walaji (Consumer Price Index), Mabadiliko ya pato la ndani la nchi (GDP) n.k . Vile vile, Bei za mahitaji ya kawaida ya walaji (Consumer Price Index) inapima gharama za bidhaa mbalimbali za msingi zinazotumiwa na kundi la watu ikiwakilisha makundi yote ya jamii kama kigezo cha upimaji wa uchumi katika nchi.

Ni muhimu kutambua kuwa, kazi ya kuangalia hali ya mfumuko wa bei katika nchi hufanywa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu.

Jambo la msingi la kujifunza ni kuwa, Katika uchumi wenye mfumuko wa bei, unashauriwa kuwekeza mara kwa mara hata kama kiasi cha kuwekeza ni kidogo. Kwa kujenga nidhamu hio, unaweza usione madhara au athari hasi za kuongezeka kwa mfumuko wa bei katika uwekezaji.

**3.3 Nini maana ya Faida Jumuishi?**

Kwa ufupi, ni faida inayopatikana kutoka katika uwekezaji ambao hugeuzwa mtaji na hivyo kutoa faida kubwa zaidi hapo baadae tofauti na uwekezaji wa muda maalum ambao faida inayopatikana inatokana tu na muda uliokaa ndani ya uwekezaji.

Je utajali ikiwa utapata faida ya asilimia 10 au 12 katika uwekezaji?

Ukweli ni kuwa, ukizingatia hilo utaweza kutengeneza tofauti kubwa katika ukuaji wa faida na mtaji kadiri muda unavyoenda/unavyoongezeka. Faida itokanayo na kompaundi inatokana na faida kuendelea kuongeza mtaji ambao huleta mapato makubwa kila mwaka. Mapato makubwa au faida kubwa au uwekezaji wa muda mrefu inaongeza kiasi cha mtaji kwa uwiano wa kijiometri.

**Matokeo ya Faida jumuishi.**

Kwa kutumia jedwali hapo chini, unaweza kuona matokeo ya nguvu ya kompaundi na faida zake kutokana na uwekezaji uliofanywa mara moja kwa kiasi cha shilingi 50,000/= na 5,000,000/= katika vipindi mbalimbali na kwa kutumia viwango tofauti vya faida.

**Jedwali Na. 09;**

| Faida | 12% | | 14% | |
|---|---|---|---|---|
| **Mwaka/Kiasi** | **50,000/=** | **5,000,000/=** | **50,000/=** | **5,000,000/=** |
| 1 | 56,000.00 | 5,600,000.00 | 57,000.00 | 5,700,000.00 |
| 3 | 70,246.40 | 7,024,640.00 | 74,077.20 | 7,407,720.00 |
| 5 | 88,117.08 | 8,811,708.42 | 96,270.73 | 9,627,072.91 |
| 10 | 155,292.41 | 15,529,241.04 | 185,361.07 | 18,536,106.57 |
| 20 | 482,314.65 | 48,231,465.47 | 687,174.49 | 68,717,449.36 |

Jedwali namba 10, linaonesha matokeo ya nguvu ya kompaundi kutokana na faida zake kwa uwekezaji uliofanywa mara moja kwa kiasi cha shilingi milioni hamsini (50) na shilingi milioni mia moja (100) katika vipindi mbalimbali na kwa kutumia viwango tofauti vya faida.

**Jedwali Na. 10;**

| Faida | 12% | | 14% | |
|---|---|---|---|---|
| **Mwaka/ Kiasi** | **50,000,000/=** | **100,000,000/=** | **50,000,000/=** | **100,000,000/=** |
| 1 | 56,000,000.00 | 112,000,000.00 | 57,000,000.00 | 114,000,000.00 |
| 3 | 70,246,400.00 | 140,492,800.00 | 74,077,200.00 | 148,154,400.00 |
| 5 | 88,117,084.16 | 176,234,168.32 | 96,270,729.12 | 192,541,458.24 |
| 10 | 155,292,410.42 | 310,584,820.83 | 185,361,065.71 | 370,722,131.41 |
| 20 | 482,314,654.66 | 964,629,309.33 | 687,174,493.59 | 1,374,348,987.19 |

Nguvu ya kompaundi na faida yake inaoneshwa kwenye majedwali yafuatayo kwa mwekezaji anaewekeza kiasi cha shilingi 50,000/=, 100,000/=, 500,000/=, na shilingi milioni 1 kwa kila mwezi kwa kutumia viwango tofauti vya faida.

**Jedwali Na. 11;** Uwekezaji wa shilingi 50,000/= kila mwezi kwa kutumia viwango tofauti vya faida.

| Awamu za kuweka pesa | Faida / Mwaka | 10% | 12% | 14% |
|---|---|---|---|---|
| 12 | 1 | 628,278.40 | 634,125.15 | 640,037.27 |
| 36 | 3 | 2,089,091.05 | 2,153,843.92 | 2,221,139.98 |
| 60 | 5 | 3,871,853.61 | 4,083,483.49 | 4,309,756.26 |
| 120 | 10 | 10,242,248.95 | 11,501,934.47 | 12,953,445.60 |
| 240 | 20 | 37,968,441.80 | 49,462,768.27 | 65,058,300.25 |

**Jedwali Na. 12;** Uwekezaji wa shilingi 100,000/= kila mwezi kwa kutumia viwango tofauti vya faida.

| Awamu za kuweka pesa | Faida / Mwaka | 10% | 12% | 14% |
|---|---|---|---|---|
| 12 | 1 | 1,256,556.81 | 1,268,250.30 | 1,280,074.54 |
| 36 | 3 | 4,178,182.11 | 4,307,687.84 | 4,442,279.95 |
| 60 | 5 | 7,743,707.22 | 8,166,966.99 | 8,619,512.51 |
| 120 | 10 | 20,484,497.89 | 23,003,868.95 | 25,906,891.21 |
| 240 | 20 | 75,936,883.60 | 98,925,536.54 | 130,116,600.51 |

Watoto Fund
Faraja kwa Watoto

**Jedwali Na. 13;** Uwekezaji wa shilingi 500,000/= kila mwezi kwa kutumia viwango tofauti vya faida.

| Awamu za kuweka pesa | Faida / Mwaka | 10% | 12% | 14% |
|---|---|---|---|---|
| 12 | 1 | 6,282,784.05 | 6,341,251.51 | 6,400,372.68 |
| 36 | 3 | 20,890,910.55 | 21,538,439.18 | 22,211,399.75 |
| 60 | 5 | 38,718,536.09 | 40,834,834.93 | 43,097,562.55 |
| 120 | 10 | 102,422,489.45 | 115,019,344.73 | 129,534,456.05 |
| 240 | 20 | 379,684,417.99 | 494,627,682.69 | 650,583,002.53 |

**Jedwali Na. 14;** Uwekezaji wa shilingi 1,000,000/= kila mwezi kwa kutumia viwango tofauti vya faida.

| Awamu za kuweka pesa | Faida / Mwaka | 10% | 12% | 14% |
|---|---|---|---|---|
| 12 | 1 | 12,565,568.09 | 12,682,503.01 | 12,800,745.36 |
| 36 | 3 | 41,781,821.09 | 43,076,878.36 | 44,422,799.50 |
| 60 | 5 | 77,437,072.17 | 81,669,669.86 | 86,195,125.10 |
| 120 | 10 | 204,844,978.90 | 230,038,689.46 | 259,068,912.10 |
| 240 | 20 | 759,368,835.99 | 989,255,365.39 | 1,301,166,005.06 |

Watoto Fund
Faraja kwa Watoto

Kutokana na jedwali hapo juu, utagundua kuwa sio busara kupoteza muda na pesa. Inabidi utambue kuwa, MUDA ni kigezo muhimu katika kufanya maajabu ya kompaundi.

**Jambo la msingi la kujifunza:**

(1) Wakati wote, tumia fursa zilizopo katika uwekezaji kwa kuzingatia mambo makuu matatu ambayo ni; usalama, ukwasi pamoja na kiwango cha faida.

(2) Endelea kuwekeza kwa muda mrefu ili unufaike na maajabu ya kompaundi.

Taasisi ya UTT AMIS inatarajia kuanza kupokea na kujibu malalamiko, maswali au maoni ya wawekezaji kidijitali (Digital Portal). Aidha, kwa sasa mwekezaji anaweza kuwasiliana nasi kwa kutuma ujumbe kwenda namba ya **WhatsApp +255 753 999 113** na kisha kupata majibu ya maswali au maelezo anayoyahitaji.

Vilevile, kupitia ukurasa wetu wa tovuti **www.uttamis.co.tz**, mwekezaji anaweza kutupata na kuhudumiwa kupitia jukwaa la **Chatbot**.

| 4.0 | **Mawasiliano** | Kwa maelezo zaidi kuhusu Mifuko yetu, tafadhali wasiliana nasi kwa anuani zifuatayo: |
|---|---|---|

**Ofisi ya UTT DAR ES SALAAM**
Ofisi za UTT AMIS Dar es Salaam
Afisa Mtendaji Mkuu,
UTT AMIS Plc,
Ghorofa ya Pili (2), Jengo la Sukari, Mtaa wa Sokoine Drive na Ohio,
S.L.P 14825, Dar es Salaam
Simu Namba: +255 (0) 22 2128460
Namba za Bure: 0800112020
Nukushi: +255 (0) 22 2137593
Barua Pepe: uwekezaji@uttamis.co.tz
Tovuti: www.uttamis.co.tz

**Ofisi ya UTT AMIS MBEYA**
Ghorofa ya Pili, Jengo la NHIF, Mbeya
S.L.P 1210, Mbeya,
Simu Namba: +255 (0) 25 2500371
Nukushi: +255 (0) 22 2137593
Barua Pepe: uwekezaji@uttamis.co.tz

**Ofisi ya UTT AMIS MWANZA**
Mezzanine, Jengo la NSSF Commercial Complex
S.L.P 640, Mwanza,
Simu Namba: +255 (0) 28 2505072
Nukushi: +255 (0) 22 2137593
Barua Pepe: uwekezaji@uttamis.co.tz

**Ofisi ya UTT AMIS DODOMA**
Ghorofa ya Sita, Jengo la PSSSF,
Mtaa wa Makole,
S.L.P 1310, Dodoma
Simu Namba: +255 (0) 26 2323861
Nukushi: +255 26 2323862
Barua Pepe: uwekezaji@uttamis.co.tz

**Ofisi ya UTT AMIS ARUSHA**
Ghorofa ya Nne, Jengo la Ngorongoro Conservation,
S.L.P 2490, Arusha,
Simu Namba: +255 (0) 27 2970625
Nukushi: +255 (0) 22 2137593
Barua Pepe: uwekezaji@uttamis.co.tz

**Ofisi ya UTT AMIS ZANZIBAR**
Ghorofa ya Tatu, Jengo la Sheikh Thabit Kombo- Michenzani
S.L.P 2190, Zanzibar
Simu Namba: +255 (0) 24 2941274
Nukushi: +255 (0) 22 2137593
Barua Pepe: uwekezaji@uttamis.co.tz

**Ofisi ya MOROGORO**
Ghorofa ya Tatu, Jengo la Shirika la Nyumba
Barabara ya Dar es Salaam
Simu Namba: 0800 112020
Barua Pepe: uwekezaji@uttamis.co.tz

**Ofisi ya KAHAMA**
Jengo la NSSF Mafao,
Simu Namba: 0800 112020
Barua Pepe: uwekezaji@uttamis.co.tz

**Ofisi ya DAR ES SALAAM**
Ghorofa ya chini
Jengo la PSSSF Complex
Barabara ya Sam Nujoma
S.L.P 14825
Dar es Salaam
Simu Namba: Toll free 0800112020
Barua Pepe. uwekezaji@uttamis.co.tz

Watoto Fund
Faraja kwa Wa...

# Watoto Fund

Faraja kwa Watoto

# Mfuko Wa Watoto

# Faraja kwa Watoto!

---

## Mifuko Mingine ya Kampuni ya Uwekezaji ya UTT AMIS

UMOJA FUND

Jikimu Income Scheme
Live Well ...You Deserve It

UKWASI FUND
Uhuru kwa mwekezaji

Wekeza Maisha
Invest Life

BOND FUND
More ideas for your money